JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE (CSEE) 2022

# KISWAHILI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE (CSEE) 2022

# 021 KISWAHILI

*Kimechapishwa na*:
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam,Tanzania.

© **Baraza la Mitihani la Tanzania, 2023**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

DIBAJI ..... iv
1.0 UTANGULIZI ..... 1
2.0 TATHMINI KWA KILA SWALI ..... 2
2.1 SEHEMU A: MASWALI YA KUCHAGUA NA KUOANISHA ..... 2
2.1.1 Swali la 1: Kuchagua ..... 2
2.1.2 Swali la 2: Kuoanisha ..... 13
2.2 SEHEMU B: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI ..... 16
2.2.1 Swali la 3: Uundaji wa Maneno ..... 16
2.2.2 Swali la 4: Fasihi Simulizi ..... 20
2.2.3 Swali la 5: Mjengo wa Tungo ..... 24
2.2.4 Swali la 6: Fasihi Simulizi ..... 28
2.2.5 Swali la 7: Maendeleo ya Kiswahili ..... 32
2.2.6 Swali la 8: Ufahamu ..... 36
2.3 SEHEMU C: MASWALI YA MAJIBU MAREFU ..... 41
2.3.1 Swali la 9: Uandishi wa Insha ..... 41
2.3.2 Swali la 10: Uhakiki wa Ushairi ..... 46
2.3.3 Swali la 11: Uhakiki wa Riwaya ..... 51
2.3.4 Swali la 12: Uhakiki wa Tamthiliya ..... 58
3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA ..... 66
4.0 HITIMISHO ..... 67
5.0 MAPENDEKEZO ..... 68
KIAMBATISHO A: UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA MWAKA 2022 ..... 70
KIAMBATISHO B: ULINGANIFU WA UFAULU KATIKA MADA MWAKA 2021 & 2022 ..... 71

# DIBAJI

Taarifa ya Uchambuzi wa Majibu ya Watahiniwa katika Mtihani wa Kitaifa wa Kidato cha Nne mwaka 2022 imeandaliwa ili kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, watunga sera, wakuza mitaala na wadau mbalimbali wa elimu kuhusu matokeo ya watahiniwa katika somo la Kiswahili kwa ujumla.

Taarifa hii ni tathmini ya mwisho inayolenga kuonesha mafanikio ya mfumo wa elimu katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa watahiniwa wa Kidato cha Nne. Kimsingi uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani huu unalenga kuonesha dhahiri maarifa ambayo mfumo wa elimu uliweza au haukuweza kuwapa watahiniwa katika somo la Kiswahili kwa kiwango cha Sekondari, Kidato cha Kwanza hadi cha Nne.

Uchambuzi uliowasilishwa katika taarifa hii una lengo la kuonesha sababu za watahiniwa kufanya vizuri, vibaya au kwa kiwango cha wastani katika maswali/mada mbalimbali zilizopimwa. Ripoti hii inaonesha baadhi ya sababu zilizofanya watahiniwa kufanya vizuri kama vile kuwa na uelewa mzuri wa mada na uzingatiaji mkubwa wa matakwa ya swali. Pia sababu za watahiniwa kuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu zimeelezwa kuwa ni pamoja na kutoa majibu yasiyojitosheza. Aidha, sababu zilizofanya watahiniwa wachache kupata alama hafifu katika majibu yao zimefafanuliwa kama vile kutoelewa matakwa ya swali, uwezo mdogo wa kuelezea dhana mbalimbali kwa ufasaha, na udhaifu katika kuelewa dhana zinazohusiana na somo la Kiswahili kwa ujumla.

Baraza la Mitihani lina imani kuwa, mrejesho uliotolewa utawawezesha wadau wote wa elimu kuchukua hatua madhubuti za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, hatimaye kuondoa changamoto zilizobainishwa katika taarifa hii. Pia Baraza linaamini kuwa, mapendekezo yaliyotolewa mwishoni mwa taarifa hii yakizingatiwa ipasavyo, kiwango cha ufaulu katika somo hili kitakuwa bora zaidi katika mitihani ijayo inayotolewa na Baraza la Mitihani.

Mwisho, Baraza la Mitihani linatoa shukrani za dhati kwa wote walioshiriki katika mchakato wa uandishi wa taarifa hii.

Dkt. Said A. Mohamed
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inachambua viwango vya ufaulu wa watahiniwa katika mtihani wa Kidato cha Nne mwaka 2022 kwa somo la Kiswahili. Mtihani huo ulikuwa na jumla ya maswali 12 yaliyogawanywa katika sehemu A, B na C kutoka katika mada za *Ufahamu*, *Matumizi ya Sarufi*, *Utumizi wa Lugha*, *Uandishi*, *Maendeleo ya Kiswahili*, pamoja na *Fasihi*. Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu A na B, na maswali matatu (3) kutoka sehemu C.

Viwango vya ufaulu wa watahiniwa vilipangwa katika madaraja mbalimbali ya ufaulu ambapo daraja A hadi D yalitumika kuwakilisha asilimia ya ufaulu wa watahiniwa waliopata alama 30 na zaidi. Aidha, daraja F lilitumika kuwakilisha asilimia ya ufaulu wa watahiniwa waliofeli yaani waliopata alama chini ya 30. Jedwali Na. 1 linaonesha ulinganifu wa ufaulu wa watahiniwa kwa kila daraja kwa mwaka 2021 na 2022.

**Jedwali Na. 1: Ufaulu wa Watahiniwa kwa kila Daraja kwa CSEE 2021 na 2022**

| **Mwaka** | **Waliofanya** | **Waliofaulu** (%) | **Gredi za Ufaulu** (%) | | | | **Waliofeli** (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **A** | **B** | **C** | **D** | **F** |
| 2021 | 487,475 | 95.58 | 3.84 | 16.64 | 53.13 | 21.42 | 4.39 |
| 2022 | 522,082 | 95.58 | 3.53 | 13.74 | 56.34 | 21.67 | 4.41 |

Katika **Jedwali Na. 1**, takwimu zinaonesha kuwa asilimia ya ufaulu wa watahiniwa kwa mwaka 2022 ilipungua katika madaraja ya juu ya ufaulu yaani daraja A na B kwa asilimia 0.31 na 2.9 mtawalia. Aidha, ufaulu uliongezeka katika daraja C na D kwa asilimia 3.1 na 0.25 mtawalia. Hata hivyo, watahiniwa waliopata alama za daraja la chini waliongezeka kwa asilimia 0.2 kutoka asilimia 4.39 ya waliopata daraja hilo mwaka 2021, hivyo kufanya wafikie asilimia 4.41.

Uchambuzi umefanyika ili kubainisha jinsi maswali yalivyojibiwa, namna yalivyopaswa kujibiwa na changamoto zilizojitokeza. Wakati wa uchambuzi viwango vitatu vya ufaulu ambavyo ni *vizuri*, *wastani* na *hafifu* vilizingatiwa.

Kiwango kizuri cha ufaulu ni alama 65 hadi 100, wastani alama 30 hadi 64 na kiwango hafifu ni 0 hadi alama 29. Aidha, chati na majedwali mbalimbali yametumika kufafanua viwango vya ufaulu ambapo katika kila chati, rangi *nyekundu* inawakilisha ufaulu hafifu, *njano* ufaulu wa wastani na *kijani* ufaulu mzuri. Hata hivyo, sampuli za majibu ya watahiniwa zimeambatanishwa katika kila swali ili kuthibitisha maelezo ya uchambuzi.

Kwa ujumla, uchambuzi huu unalenga kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa walimu, wanafunzi na wadau wengine wa elimu. Pia utasaidia kuweka mikakati ya kutatua changamoto zilizojitokeza katika mtihani huu na kuimarisha ufaulu ili uwe wa juu katika mitihani ijayo.

## 2.0 TATHMINI KWA KILA SWALI

Sehemu hii inachambua kwa kina majibu ya kila swali yaliyotolewa na watahiniwa kwa kuonesha maswali yaliyokuwa na ufaulu mzuri, ufaulu wa wastani na yale yaliyokuwa na ufaulu hafifu. Aidha, sababu za ufaulu wa watahiniwa katika makundi hayo zimeelezwa bayana kwa kila swali.

### 2.1 SEHEMU A: MASWALI YA KUCHAGUA NA KUOANISHA


Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili (2) ambapo swali la kwanza (1) lilikuwa la kuchagua likiwa na vipengele kumi (10) na swali la pili (2) lilikuwa la kuoanisha maana na dhana katika orodha A na B. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 15.

#### 2.1.1 Swali la 1: Kuchagua

Swali hili lililenga kupima uelewa wa watahiniwa juu ya dhana mbalimbali zinazohusu mada anuwai za somo la Kiswahili. Swali lilihusu mada ya *Aina za Maneno*, *Mawasiliano na Utumizi wa Lugha*, *Mjengo wa Tungo*, *Uandishi* na *Uhakiki/Uhifadhi wa Kazi za Fasihi Simulizi*. Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kuchagua herufi ya jibu sahihi kutoka katika machaguo matano (A - E) kwa kila kipengele.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 522,082 (100%) ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Swali lilikuwa miongoni mwa maswali

yaliyojibiwa vizuri sana ambapo watahiniwa wengi (435,564) sawa na asilimia 83.43 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 1 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 1**: *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 1*

Katika Chati Na. 1, watahiniwa 58,069 (11.12%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 6.5 hadi 10, watahiniwa 377,495 (72.31%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 3 hadi 6 na watahiniwa 86,518 (16.57%) walifeli kwa kupata alama 0 hadi 2.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika vipengele vingi unaonesha kuwa asilimia 72.31 walifaulu kwa kiwango cha wastani kutokana na kukosa umahiri wa kutosha kuhusu dhana mbalimbali zilizotahiniwa kwa baadhi ya vipengele. Watahiniwa hao walimudu kuchagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele 3 - 6 na kupata alama za wastani.

Aidha, watahiniwa wachache (11.12%) walijibu vizuri swali hili kwa kuwa walikuwa na umahiri wa dhana zilizotahiniwa katika mada husika. Kwa ujumla, watahiniwa hao waliweza kujibu vipengele vingi vya swali hili kwa kuchagua herufi yenye jibu sahihi. Kielelezo Na. 1.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya

mwanafunzi aliyeweza kuchagua majibu sahihi katika vipengele (i - x) na kupata alama zote 10.

| i | ii | iii | iv | v | vi | vii | viii | ix | x |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| C | E | B | B | E | D | D | A | C | B |

Kielelezo Na. 1.1: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 1.

Kielelezo Na.1.1, kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuchagua herufi za majibu sahihi kutokana na kuwa na uelewa wa kutosha wa dhana mbalimbali za mada zilizotahiniwa katika swali hili.

Hata hivyo, watahiniwa wengine (16.57%) waliojibu swali hili walichagua majibu yasiyo sahihi katika vipengele vingi, hivyo kupata alama hafifu. Baadhi yao walionesha kutokuelewa vyema dhana zilizotahiniwa katika swali hili. Uchambuzi zaidi kuhusu namna watahiniwa walivyojibu vipengele mbalimbali vya swali hili umefafanuliwa kama ifuatavyo:

*(i)* *"Kushindana na mtu aliyekuzidi kwa kila hali si busara". Methali zifuatazo zinashabihisha kauli hii* ***isipokuwa****:*

*A* *Mwenye pesa si mwenzio*
*B* *Nazi haishindani na jiwe*
*C* *Chanda chema, huvikwa pete*
*D* *Mwenye nguvu mpishe*
*E* *Maji yakija kasi yapishe*

Swali hili lilitoka katika mada ya *Fasihi Simulizi*, mada ndogo ya *Ufafanuzi wa Vipera vya Tanzu za Fasihi Simulizi.* Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kuelewa maana na mafunzo yanayopatikana kwenye methali alizopewa katika machaguo na jinsi zinavyoweza kuhusiana na kauli iliyopo katika swali. Hivyo, mtahiniwa alipaswa kuchagua methali isiyoendana na kauli "kushindana na mtu aliyekuzidi kwa kila hali si busara." Watahiniwa waliojibu kwa usahihi swali hili walichagua herufi C *Chanda chema huvikwa pete* ambayo ni methali sahihi isiyoendana

na kauli hiyo. Watahiniwa hao walionesha kuwa na uelewa wa kutosha wa kipera cha methali.

Watahiniwa walioshindwa kuchagua herufi ya jibu sahihi katika kipengele hiki walichagua vipotoshi A *Mwenye pesa si mwenzio;* B *Nazi haishindani na jiwe;* D *Mwenye nguvu mpishe*; na E *Maji yakija kasi yapishe* kutokana na kukosa uelewa wa kutosha kuhusu maana au mafunzo yanayopatikana katika methali hizo. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa, watahiniwa walishindwa kung'amua kuwa maana na ujumbe uliopo katika methali hizo zinashabihiana na kauli "kushindana na mtu aliyekuzidi kwa kila hali si busara."

*(ii)* *Neno linaloingizwa katika kamusi kwa wino uliokolezwa, fasili, matamshi na aina ya neno hilo kwa pamoja huitwaje?*

*A* *Kidahizo*
*B* *Kategoria*
*C* *Fasili*
*D* *Istilahi*
*E* *Kitomeo*

Swali hili lilitoka katika mada ya *Aina za Maneno* na mada ndogo ya *Matumizi ya Kamusi.* Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa kukumbuka matumizi sahihi ya kamusi. Watahiniwa waliokuwa na umahiri huo walichagua herufi ya jibu sahihi E *Kitomeo* ambalo ni neno linaloingizwa katika kamusi kwa wino uliokolezwa lenye fasili, pamoja na matamshi na aina ya neno husika.

Hata hivyo, baadhi ya watahiniwa waliojibu swali hili hawakuonesha kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu matumizi ya kamusi kwani walichagua vipotoshi A *Kidahizo,* B *Kategoria,* C *Fasili,* na E *Istilahi*. Watahiniwa hao walishindwa kubaini kuwa kitomeo ni neno linaloingizwa katika kamusi kwa wino uliokolezwa pamoja na fasili, matamshi na aina ya neno husika. Uchaguzi wa kipotoshi A *Kidahizo* ulitokana na watahiniwa hao kuchanganya dhana ya *kidahizo* na *kitomeo* ambapo kidahizo ni

neno linaloingizwa katika kamusi kwa chapa iliyokoza, au kwa rangi, kubwa na tofauti kidogo na ni neno kuu katika kamusi. Uchaguzi wa kipotoshi B *Kategoria* ulitokana na kukosa uelewa wa neno hilo lenye maana ya jumla ya vitu vya aina fulani vinavyoweza kuwekwa pamoja kwa kuzingatia sifa zinazofanana. Uchaguzi wa kipotoshi C *Fasili* ulitokana na watahiniwa hao kushindwa kuelewa kuwa fasili ni ufafanuzi wa neno kwa lugha ya mjazo. Uchaguzi wa kipotoshi D *Istilahi* kilitokana na kutokuelewa kuwa istilahi ni dhana fulani katika uwanja maalum wa kitaaluma na haihusiani na matumizi ya kamusi kwa ujumla.

*(iii) Kikundi cha maneno kinachoonesha jambo lililotendwa na mtenda katika sentensi hujulikanaje?*

*A Chagizo*
*B Kitenzi*
*C Kivumishi*
*D Shamirisho*
*E Nomino*

Swali hili lilitoka katika mada ya *Mjengo wa Tungo* na lililenga kupima maarifa ya mtahiniwa katika kutambua dhima na matumizi ya maneno katika sentensi. Watahiniwa waliojibu kwa usahihi swali hili walichagua herufi ya jibu sahihi B *Kitenzi*. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu kitenzi ambacho hufanya kazi ya kueleza kitendo kilichotendwa na mtenda katika sentensi.

Baadhi ya watahiniwa walionesha kukosa maarifa ya kutosha juu ya dhana ya kitenzi na dhima yake katika sentensi, hivyo kuchagua vipotoshi A *Chagizo*, C *Kivumishi*, D *Shamirisho* na E *Nomino*. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo ulitokana na kukosa maarifa kuwa A *Chagizo* ni dhana ya uainishaji wa aina za maneno katika kikundi kinachokaliwa na vielezi; C *Kivumishi* ni aina ya neno linalotoa sifa bainifu za nomino; D *Shamirisho* ni dhana ya uainishaji wa aina za maneno yanayorejelea nomino inayojitokeza upande wa kiarifu ambapo neno kuu ni kitenzi na uchaguzi wa kipotoshi na E *Nomino* hawakujua kuwa ni neno linalotaja jina la mahali, mtu,

kitu, hali au tendo. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unadhihirisha wazi kuwa watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya aina za maneno, hivyo kushindwa kubaini kitenzi ambacho hufanya kazi ya kueleza kitendo kilichotendwa na mtenda au mtendwa katika sentensi.

*(iv)* *Bainisha sentensi yenye vielezi zaidi ya kimoja katika sentensi zifuatazo:*

*A* *Vitabu vyangu vyote vimeibiwa na watoto wako.*

*B* *Mbuzi aliyepotea jana ameonekana leo asubuhi.*

*C* *Shule ngapi zinaweza kushiriki mashindano?*

*D* *Wengi walikuwa wanataka kwenda masomoni.*

*E* *Wanakijiji hawa wamefanya uchaguzi kwa amani.*

Swali hili lilitoka katika mada ya *Aina za Maneno* na mada ndogo ya *Matumizi ya Aina za Maneno katika Tungo* na lililenga kupima maarifa ya mtahiniwa katika kutambua aina za maneno katika tungo. Watahiniwa waliokuwa na umahiri wa kutosha kuhusu matumizi ya vielezi katika sentensi walichagua herufi ya jibu sahihi *B*: *Mbuzi aliyepotea jana ameonekana leo asubuhi* ambapo vielezi vilikuwa ni *leo* na *asubuhi*.

Wapo watahiniwa walioshindwa kubaini sentensi yenye vielezi zaidi ya kimoja katika sentensi walizopewa. Watahiniwa hao walichagua vipotoshi A *Vitabu vyangu vyote vimeibiwa*; C *Shule ngapi zinaweza kushiriki mashindano*; D *Wengi walikuwa wanataka kwenda masomoni*; na E *Wanakijiji hawa wamefanya uchaguzi kwa amani*. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo ulitokana na kukosa uelewa wa kutosha kuhusu aina za maneno, hivyo kushindwa kutofautisha vielezi na aina zingine za maneno zilizotumika kuunda sentensi hizo. Kwa ujumla, sentensi zilizopo katika vipotoshi A, C na E hazikuwa na kielezi chochote. Aidha, kipotoshi *D* kilikuwa na kielezi kimoja tu *masomoni* kinyume na matakwa ya swali kwani mtahiniwa alitakiwa kubainisha sentensi yenye vielezi zaidi ya kimoja katika sentensi hizo.

(v) *Pande mbili zinazohusika kwenye lugha ya maandishi ni zipi?*

*A Mwandishi na msikilizaji*
*B Msikilizaji na msomaji*
*C Mwandishi na mzungumzaji*
*D Msomaji na msimuliaji*
*E Msomaji na mwandishi*

Swali hili lilitoka katika mada ya *Mawasiliano* na lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa kuhusu aina za lugha. Baadhi ya watahiniwa waliojibu swali hili walionesha kuwa na uelewa wa kutosha wa aina za lugha na sifa bainifu za aina hizo, hivyo kuchagua herufi ya jibu sahihi E *Msomaji na mwandishi*.

Hata hivyo, watahiniwa wengine walichagua vipotoshi A *Mwandishi na msikilizaji*; B *Msikilizaji na msomaji*; C *Mwandishi na mzungumzaji*; na D *Msomaji na msimuliaji* kwa kuwa hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu lugha ya maandishi na lugha ya mazungumzo hivyo kushindwa kutambua pande mbili za lugha ya maandishi ambazo ni *msomaji* na *mwandishi*. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo ulitokana na watahiniwa hao kukosa uelewa kuwa maneno "msikilizaji", "mzungumzaji" na "msimuliaji" yaliyopo katika seti za vipotoshi A, B, C na D yanahusu lugha ya mazungumzo na siyo lugha ya maandishi. Pia *msimuliaji* ni fanani katika kazi za fasihi simulizi.

(vi) *Dhima ya vigelegele katika utendekaji wa sanaa za maonesho ni ipi?*

*A Kuishirikisha na kuiondolea hadhira udhia wa kumsikiliza mtu mmoja.*
*B Hadhira kukata shauri juu ya mwendo wa kazi za sanaa za maonesho.*
*C Kuweka alama za mapigo ya kimuziki katika kazi ya sanaa za maonesho.*
*D Kuonesha upeo wa furaha na burudani ya kazi ya sanaa za maonesho.*
*E Kuonesha mbwembwe katika kazi ya sanaa za maonesho.*

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Simulizi*, mada ndogo ya *Sanaa za Maonesho* kama utanzu wa fasihi simulizi na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa kuhusu uhakiki wa kazi za fasihi simulizi. Baadhi ya watahiniwa walichagua jibu sahihi D *Kuonesha upeo wa furaha na burudani ya kazi ya sanaa za maonesho*. Watahiniwa hao walionesha kuwa na ujuzi na maarifa ya kutosha kuhusu dhima ya vigelegele katika sanaa za maonesho.

Kwa upande mwingine, baadhi ya watahiniwa walioshindwa kujibu swali hili walichagua vipotoshi A *Kuishirikisha na kuiondolea hadhira udhia wa kumsikiliza mtu mmoja*; B *Hadhira kukata shauri juu ya mwendo wa kazi za sanaa za maonesho*; C *Kuweka alama za mapigo ya kimuziki katika kazi ya sanaa za maonesho*; na E *Kuonesha mbwembwe katika kazi ya sanaa za maonesho*. Watahiniwa hao walikosa maarifa kuhusu dhima ya vigelegele katika utendekaji wa sanaa za maonesho ambayo ni kuonesha upeo wa furaha na burudani ya kazi ya sanaa za maonesho.

*(vii)* *Njia ipi hutunza sauti pamoja na vidokezo vyake katika kuhifadhi kazi ya fasihi simulizi kati ya hizi?*

*A* *Maandishi*
*B* *Kanda ya filamu*
*C* *Mitandao*
*D* *Kinasa sauti*
*E* *Masimulizi*

Swali lilitoka katika mada ya *Uhifadhi wa Kazi za Fasihi Simulizi*, mada ndogo ya *Njia za kuhifadhi Fasihi Simulizi*. Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa kuelewa njia za kuhifadhi kazi za fasihi simulizi. Watahiniwa waliojibu vizuri swali hili walidhihirisha kuwa na uelewa wa kutosha juu ya uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi hivyo kuchagua herufi ya jibu sahihi D *Kinasa sauti* kuwa ndiyo njia pekee inayotunza sauti pamoja na vidokezo vyake katika kuhifadhi kazi za fasihi simulizi.

Kwa upande mwingine, baadhi ya watahiniwa walikosa uelewa wa kutosha juu ya njia za uhifadhi wa kazi ya fasihi simulizi hivyo

kuchagua vipotoshi A, B, C, na E. Uchaguzi wa kipotoshi A *Maandishi* ulitokana na watahiniwa hao kutoelewa kuwa maandishi ni moja ya njia za kuhifadhi kazi ya fasihi simulizi isiyoweza kutunza sauti pamoja na vidokezo vyake. B *Kanda ya filamu* ulitokana na watahiniwa hao kukosa uelewa kuwa mikanda ya filamu hutunza sauti pamoja na vitendo vinavyotendeka katika kazi ya fasihi simulizi kinyume na matakwa ya swali. Uchaguzi wa kipotoshi C *Mitandao* ulitokana na watahiniwa hao kushindwa kuelewa kuwa *mitandao* ni mfumo wa mawasiliano ya kielektroniki unaopitia katika kompyuta ili kuwasiliana au kupeana taarifa. Kipotoshi E *Masimulizi,* ulitokana na watahiniwa hao kukosa uelewa kuwa masimulizi ni maelezo yanayotolewa kuhusu namna tukio fulani lilivyotokea katika kipindi fulani cha maisha na siyo njia ya kuhifadhi kazi za fasihi simulizi.

*(viii) Jambo gani muhimu huzingatiwa na mtunzi wa insha ya hoja?*

*A Lugha yenye ukinzani*
*B Lugha isiyo na mvuto*
*C Lugha ya kisanaa*
*D Lugha ya kufikirisha*
*E Lugha inayosifia*

Swali lilitoka katika mada ya *Uandishi* na mada ndogo ya *Uandishi* wa *Insha za Hoja* na lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika uandishi wa insha yenye kutetea mawazo ya aina fulani na kuyapinga mengine kwa uthibitisho dhahiri (insha ya hoja). Watahiniwa waliioonesha umahiri huo walichagua herufi ya jibu sahihi A *Lugha yenye ukinzani* ambalo ndilo jambo la muhimu linalozingatiwa katika uandishi wa insha ya hoja.

Aidha, baadhi ya watahiniwa ambao hawakuwa na umahiri katika uandishi wa insha za hoja walichagua vipotoshi B *Lugha isiyo na mvuto*; C *Lugha ya kisanaa*; D *Lugha ya kufikirisha*; na E *Lugha inayosifia* visivyokidhi matakwa ya swali. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa watahiniwa hao walikosa maarifa ya kutosha juu ya utunzi wa insha ya hoja, hivyo kushindwa kuelewa

kuwa lugha yenye ukinzani ndio jambo muhimu la kuzingatiwa na mtunzi wa insha ya hoja. Hata hivyo, baadhi ya sifa zilizopo katika vipotoshi hivyo ni muhimu katika uandishi wa insha yoyote lakini lugha yenye ukinzani ndiyo sifa pekee ya utunzi wa insha ya hoja.

*(ix)* *Zifuatazo ni kazi za alama ya uandishi nuktamkato (;)* ***isipokuwa****:*

*A* *Kuonesha kuwa vitu vinavyofuata viko katika orodha.*
*B* *Kuunga mawazo mawili tofauti katika sentensi.*
*C* *Kuonesha kwamba kinachofuata ni ufafanuzi zaidi.*
*D* *Kuunga mawazo mawili au zaidi katika sentensi.*
E *Kutenga vifungu vya sentensi ambavyo ni virefu.*

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uandishi*, mada ndogo ya *Kutumia Alama za Uandishi* na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa kuelewa kazi ya alama ya uandishi *nuktamkato* (;). Watahiniwa waliojibu vizuri swali hili walikuwa na uelewa wa kutosha wa alama za uandishi hivyo kuchagua herufi ya jibu sahihi C *Kuonesha kwamba kinachofuata ni ufafanuzi zaidi* ambayo si kazi ya alama ya uandishi *nuktamkato* (;).

Hata hivyo, baadhi ya watahiniwa waliofanya mtihani huu walishindwa kujibu swali hili kutokana na kukosa maarifa ya kutosha juu ya kazi za alama za uandishi, hivyo kuchagua vipotoshi A *Kuonesha kuwa vitu vinavyofuata viko katika orodha*; B *Kuunga mawazo mawili tofauti katika sentensi*; D *Kuunga mawazo mawili au zaidi katika sentensi*; na E *Kutenga vifungu vya sentensi ambavyo ni virefu*. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo ulitokana na watahiniwa kushindwa kubaini kuwa hizo zote ni kazi zinazofanywa na alama ya nuktamkato (;) katika sentensi. Aidha, *kazi ya kuonesha kwamba kinachofuata ni ufafanuzi zaidi*; hufanywa na alama ya nukta mbili/pacha (:).

*(x)* *Kipi ni kipengele kinachohusu mjengeko wa kazi za fasihi?*

*A* *Mtindo*
*B* *Muundo*
*C* *Mandhari*
*D* *Wahusika*
*E* *Lugha*

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Simulizi* na lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa kuhusu vipengele vya uhakiki katika kazi za fasihi. Watahiniwa waliojibu kwa usahihi swali hili walichagua herufi ya jibu sahihi B *Muundo*, kwani walionesha kuwa na uelewa wa kutosha juu ya kipengele cha fani (muundo) ambacho ndicho kinachohusika na mjengeko wa kazi za fasihi.

Baadhi ya watahiniwa waliofanya mtihani huu walichagua vipotoshi A *Mtindo*, C *Mandhari*, D *Wahusika* na E *Lugha* kutokana na kukosa umahiri katika uhakiki wa kazi za fasihi. Watahiniwa hao walionesha kukosa uelewa kuhusu vipengele vya fani katika kazi za fasihi, hivyo kushindwa kujua kuwa muundo pekee ndio unaohusika na mjengeko wa kazi za fasihi. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unatokana na watahiniwa kutokujua kuwa, *Mtindo* unahusika na upekee wa kazi ya fasihi; *Mandhari* ni mahali/eneo ambalo tukio la kifasihi hutendeka; *Wahusika* ni watu/miti/viumbe vinavyowakilisha watendaji katika kazi ya fasihi; na *Lugha* ni mpangilio wa sauti za nasibu zenye maana na zilizokubaliwa na wanajamii zitumike katika mawasiliano. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo kwa ujumla haukukidhi matakwa ya swali hili. Kielelezo Na. 1.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili na kupata alama hafifu.

| i | ii | iii | iv | v | vi | vii | viii | ix | x |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| B | C | D | C | A | B | A | B | D | D |

Kielelezo Na. 1.2: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 1.

Kielelezo Na. 1.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kipengele hata kimoja cha swali hili kutokana na kukosa maarifa kuhusu dhana anuwai za mada zilizotahiniwa katika kipengele (i) hadi (x).

### 2.1.2 Swali la 2: Kuoanisha


Swali hili lilitoka katika mada ya *Fasihi Simulizi* na mada ndogo ya *Tamathali za Semi* na lililenga kupima umahiri wa watahiniwa kuhusu matumizi ya tamathali za semi katika kazi za fasihi. Swali liliuliza;

*Oanisha maana za tamathali za semi zilizo katika Orodha A na tamathali husika kutoka Orodha B, kisha andika herufi ya jibu sahihi katika kijitabu chako cha kujibia.*

| ***Orodha A*** | ***Orodha B*** |
|---|---|
| *(i) Ushangaaji wa jambo fulani, aghalabu huambatana na alama ya mshangao.*<br>*(ii) Upangiliaji wa maneno katika namna ya kupingana ili kusisitiza mawazo fulani.*<br>*(iii) Ulinganishaji wa vitu viwili au zaidi vyenye sifa tofauti kwa kutumia viunganishi.*<br>*(iv) Uhuishaji wa kitu kisicho binadamu kupewa uwezo wa kutenda kama binadamu.*<br>*(v) Urudiaji wa neno, herufi au silabi ili kusisitiza jambo.* | *A Tashibiha*<br>*B Takriri*<br>*C Sitiari*<br>*D Tabaini*<br>*E Tashihisi*<br>*F Nidaa*<br>*G Tanakali sauti* |

Swali lilikuwa na jumla ya vipengele vitano ambapo mtahiniwa alitakiwa kuoanisha maana za tamathali za semi zilizokuwa katika orodha A na tamathali husika katika orodha B.

Watahiniwa 522,082 sawa na asilimia 100 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walijibu swali hili. Swali hili lilikuwa na ufaulu wa wastani ambapo watahiniwa 325,918 sawa na asilimia 62.43 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 2 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.





**Chati Na. 2:** *Ufaulu wa watahiniwa katika Swali la 2*

Katika Chati Na. 2, watahiniwa 128,945 (24.70%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 3.5 hadi 5, watahiniwa 196,973 (37.73%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 1.5 hadi 3 na watahiniwa 196,164 (37.57%) walifeli kwa kupata alama 0 hadi 1.

Watahiniwa 196,973 (37.73%) waliojibu swali hili walionesha kuwa na uelewa usiojitosheleza kuhusu maana za dhana mbalimbali za tamathali za semi hivyo kupata alama za wastani. Majibu ya watahiniwa hao yalionesha kuwa baadhi walichanganya maana za tamathali za semi na tamathali husika. Kwa ujumla, majibu ya watahiniwa katika vipengele hivyo hayakuwa sahihi, hivyo kupata alama 1.5 - 3. Kiwango hiki kilitokana na watahiniwa hao kuoanisha kwa usahihi vipengele 2 hadi 3 vya swali na kushindwa kuoanisha kwa usahihi vipengele vingine.

Asilimia 24.70 ya watahiniwa waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kuwa walionesha kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu maana za tamathali za semi walizopewa. Watahiniwa hao waliweza kuoanisha kwa usahihi maana za tamathali za semi

zilizokuwa katika *Orodha A* na tamathali husika katika *Orodha B* kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 2.1.



| 2 | i | ii | iii | iv | v |
|---|---|---|---|---|---|
| | F | D | A | E | B |

Kielelezo Na. 2.1: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 2.

Kielelezo Na. 2.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuoanisha kwa usahihi maana za tamathali za semi katika Orodha A na tamathali husika zilizo katika Orodha B kwa kuandika herufi zenye tamathali za semi zinazowiana na maana halisi za tamathali za semi (i) - (v).

Kwa upande mwingine, watahiniwa 196,164 sawa na asilimia 20.39 walishindwa kuoanisha maana za tamathali za semi zilizo katika Orodha A na tamathali husika katika Orodha B kwa vipengele vingi na kupata alama hafifu (0 – 1). Baadhi yao walichagua vipotoshi C *sitiari* na G *tanakali sauti* dhana ambazo hazihusiani na maana zote za tamathali za semi zilizopo katika Orodha A. Hii ilitokana na watahiniwa hao kuwa na uelewa mdogo wa matumizi ya lugha katika kazi za fasihi hususani matumizi ya tamathali za semi. Vilevile, watahiniwa wengine walifikiri kuwa kipengele (i) *Ushangaaji wa jambo fulani, aghalabu huambatana na alama ya mshangao* hivyo kuchagua kipotoshi G *Tanakali sauti* ambayo ni tamathali ya semi yenye mwigo wa sauti ya kitu au hali mbalimbali badala ya kuchagua herufi ya jibu sahihi *F Nidaa*. Aidha, katika kipengele (iv) *Uhuishwaji wa kitu kisicho binadamu kupewa uwezo wa kutenda kama binadamu*, baadhi ya watahiniwa walichagua kipotoshi C *Sitiari* yaani ulinganishaji wa vitu viwili au zaidi bila kutumia kiunganishi *badala* ya herufi ya jibu sahihi E *Tashihisi*. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unatokana na watahiniwa hao kukosa uelewa wa kutosha juu ya vipengele vya tamathali za semi, hivyo kuchanganya matumizi ya tamathali hizo. Kielelezo Na. 2.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuoanisha kwa usahihi maana za tamathali mbalimbali za semi na tamathali husika, hivyo kupata alama 0.

| i | ii | iii | iv | v |
|---|---|---|---|---|
| B | C | E | A | G |

Kielelezo Na. 2.2*:* Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 2.

Kielelezo Na. 2.2, kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuoanisha maana za tamathali za semi katika Orodha A na tamathali husika kutoka Orodha B kutokana na kukosa uelewa wa tamathali mbalimbali za semi.


## 2.2 SEHEMU B: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI

Sehemu hii ilikuwa na maswali sita (6) yanayohitaji majibu mafupi na ilikuwa na jumla ya alama 40. Sehemu hii ilihusu mada ya *Uundaji wa Maneno, Aina za Maneno, Maendeleo ya Kiswahili, Uhakiki wa Kazi za Fasihi Simulizi* na *Ufahamu.*

### 2.2.1 Swali la 3: Uundaji wa Maneno

Swali hili lilitoka katika mada ya *Kuongeza Msamiati wa Kiswahili*, mada ndogo ya *Uundaji wa Maneno* na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa kuhusu uambishaji katika vitenzi vya Kiswahili. Swali lilimtaka mtahiniwa kufafanua taarifa nne za kisarufi zilizopo katika viambishi awali vya vitenzi vya Kiswahili na kutoa mfano kwa kila moja.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 522,082 sawa na asilimia 100 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani huu. Ni miongoni mwa maswali ambayo ufaulu wake ulikuwa wa wastani ambapo asilimia 35.38 sawa na watahiniwa (184,787) walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 3 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.





**Chati Na. 3:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 3*

Chati Na. 3 inaonesha kuwa, watahiniwa 337,347 (64.62%) walipata alama hafifu (0 hadi 1), watahiniwa 86,438 (16.56%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 1.5 hadi 2.5 na watahiniwa 98,299 (18.83%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 3 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa, zaidi ya nusu ya watahiniwa (64.62%) waliofanya mtihani huu walifeli kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 1 kutokana na kukosa umahiri juu ya mada ya viambishi, hususani viambishi awali. Watahiniwa hao walishindwa kufafanua taarifa zinazodokezwa na viambishi awali kwenye vitenzi vya Kiswahili. Kwa kukosa umahiri huo, baadhi walifafanua taarifa zinazohusu mzizi katika vitenzi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika (i) anakimbia (kimb-); (ii) anacheza (chez-); (iii) anapigwa (pig-); na (iv) analima (lim-). Aidha, wengine walibainisha kauli mbalimbali katika vitenzi kama vile *kutenda* (anapiga), kutendesha (pigisha), kutendea (chezea), kutendwa (anapigwa) na kauli nyinginezo kinyume na matakwa ya swali. Kwa ujumla, watahiniwa hao walitakiwa kufafanua taarifa nne za kisarufi zilizopo katika viambishi awali vya vitenzi vya Kiswahili na kutoa mfano kwa kila moja kati ya hizi: *kudokeza nafsi mbalimbali*, mfano, a-nasoma, kiambishi a- nafsi ya tatu umoja; *kudokeza njeo mbalimbali* mfano, wa-li-ofika, kiambishi -li- wakati ujao; *kudokeza ukanushi wa*

*tendo*; mfano, ha-chezi, kiambishi ha- hutoa taarifa ya ukanushi wa tendo; *kudokeza upatanisho wa kisarufi (ngeli* za nomino/idadi*)* mfano, tu-tavuna kiambishi tu- ni kiambishi cha nafsi/ngeli/ idadi ya wingi; na *kudokeza urejeshi wa tendo kwa mtenda/mtendwa au kitendwa*, mfano, wali –vyo- imba kiambishi -vyo- hutoa taarifa ya urejeshi wa mtenda. Kielelezo Na. 3.1 ni mfano wa jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kufafanua taarifa nne za kisarufi zilizopo katika viambishi awali vya vitenzi vya Kiswahili, hivyo akapata 0.



3
(i) Kisarufi Matamshi
hiki ni taarifa zile ambazo zina fuata wakati wa kutamka
Mfano
Meza - Mesa
Lima - Mali
(ii) Kisarufi Maumbo
Ni taarifa zinazofuata waka hi wa kuzingatia Maumbo kama vile Ukubwa wa kitu hiyi umyesha umbo lake.
(iii) Kisarufi Muundo
Ni taarifa zinazofuata waka hi wa kupangilia vizuri kazi zako
(iv) Kisarufi Maana
Ni taarifa zinazofuata wa kati wakufuata taratibu za kisarufi
Mfano
- Mama ameenda Shambani hii inaleta Maana
- Shambani mama ameenda-hii lete Maana kamili

Kielelezo Na. 3.1: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 3.

Katika Kielelezo Na. 3.1, mtahiniwa alifafanua matawi ya sarufi katika vipengele (i) hadi (iv) kinyume na matakwa ya swali kwa kuelezea *sarufi matamshi, maumbo, muundo maana*, badala ya kufafanua taarifa nne za kisarufi zilizopo katika viambishi awali vya vitenzi kama ilivyotakiwa.

Baadhi ya watahiniwa (16.56%) walikuwa na ufaulu wa wastani kutokana na kushindwa kufafanua taarifa zote nne za kisarufi zilizopo katika viambishi awali vya vitenzi vya Kiswahili, hivyo kupata alama 1.5 hadi 2.5 katika swali hili. Ufaulu huo ulitokana na kufafanua taarifa chache kwa usahihi zinazodokezwa na viambishi awali kwenye vitenzi vya Kiswahili na kushindwa kufafanua kwa usahihi taarifa zingine. Watahiniwa wengine waliweza kubainisha viambishi awali vya vitenzi kwa usahihi ila walishindwa kutoa ufafanuzi unaokidhi matakwa ya swali.

Watahiniwa wengine (98,299) sawa na asilimia 18.83 waliweza kufafanua taarifa nne za kisarufi zilizopo katika viambishi awali vya vitenzi vya Kiswahili na kupata alama za juu. Kwa ujumla, watahiniwa walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu uambishaji katika vitenzi, hivyo kufafanua kwa usahihi taarifa za viambishi awali kama ifuatavyo: *Kudokeza nafsi mbalimbali katika vitenzi* mfano, **wa**nasoma (wa)- nafsi ya tatu wingi; *Kudokeza njeo mbalimbali katika vitenzi* mfano, *a**ta**som*a (ta) - njeo ya wakati ujao; *Kudokeza ukanushi wa tendo* mfano, ***si**taki* (si)**-** ukanushi; *Kudokeza kiambishi cha upatanisho wa kisarufi kinachodokeza ngeli za nomino/idadi* mfano, ***a**nalima* (a-) upatanisho wa kisarufi; *Kudokeza urejeshi wa tendo kwa mtendwa, mtenda au kitenda* mfano, ali**cho**kula, ali**vyo**kula, ataka**ye**kula, ali**po**kula (mfano, cho-vyo-, ye- na po**-)** - urejeshi wa tendo kwa mtenda na *Kudokeza mtendwa wa jambo* mfano, ana**u**tafuta, usi**pa**fagie, wali**m**kumbatia (u-, -pa- na -m-) - mtendwa. Kielelezo Na. 3.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama za juu.



Q3. i) Huonesha nafsi ya mtenda and mtendwa
Mfano: Wanakula
Wa- huonesha nafsi tya tatu Wingi.

ii) Huonesha njeo au Wakati
Mfano: Tutafua
-ta- huonesha wakati ujao.

iii) Huonesha Uyakinishi au Ukanushi.
Mfano: Hatutakuja
Ha- huonesha hali ya Ukanushi.


iv) Huonesha Umoja na wingi.
Mfano: Anaandika
A- huonesha Umoja katika nafsi ya tatu.

Kielelezo Na. 3.2: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 3.

Katika Kielelezo Na. 3.2, mtahiniwa alifafanua kwa usahihi taarifa za viambishi awali katika vitenzi vya Kiswahili kama vile *nafsi*, *njeo*, *uyakinishi/ukanushi* na *umoja/wingi* kwa kutoa hoja na mifano iliyokidhi matakwa ya swali, hivyo alipata alama zote za swali hili.

### 2.2.2 Swali la 4: Fasihi Simulizi

Swali hili lilitoka katika mada ya *Fasihi Simulizi*, mada ndogo ya *Aina za Fasihi*. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kuelewa mambo yanayodhihirisha uhai wa fasihi simulizi. Swali lilimtaka mtahiniwa kutumia hoja nne na mifano kuthibitisha kauli kuwa "Fasihi simulizi ni hai." Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 522,082 sawa na asilimia 100 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Swali hili lilikuwa miongoni mwa maswali yaliyokuwa na kiwango hafifu cha ufaulu. Watahiniwa wachache (123,955) sawa na asilimia 23.74 pekee waliojibu swali hili ndio waliofaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 4 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.





**Chati Na. 4:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 4*

Katika Chati Na. 4, watahiniwa 398,127 (76.26%) walipata alama hafifu (0 hadi 1), watahiniwa 80,825 (15.48%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 1.5 hadi 2.5 na watahiniwa 43,129 (8.26%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 3 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa wengi (398,127) sawa na asilimia 76.26 waliojibu swali hili walifeli kwa kupata alama 0 hadi 1 kutokana na kukosa umahiri kuhusu dhana ya uhai katika fasihi simulizi. Watahiniwa hao walishindwa kuthibitisha kwa hoja nne na mifano kauli isemayo "Fasihi simulizi ni hai." Majibu yasiyo sahihi ya watahiniwa hao yanaonesha kuwa baadhi walibainisha *tanzu* na *vipera* vya fasihi simulizi na wengine walifafanua *dhima* mbalimbali za fasihi simulizi katika jamii kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: *huburudisha; huelimisha; huonya;* na *hukemea maovu*. Pia alitoa mifano inayoshadidia dhima hizo kutoka katika tamthiliya ya "Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe" na "Orodha." Jibu hilo linaonesha kuwa mtahiniwa huyo alishindwa kutofautisha uhai wa fasihi simulizi na dhima za fasihi. Mtahiniwa huyo alitakiwa kuthibitisha kauli "fasihi simulizi ni hai" kwa kueleza hoja zifuatazo: *kuwepo kwa utendekaji kati ya hadhira na fanani,*

*kuonana ana kwa ana kati ya hadhira na fanani, kubadilika kulingana na mazingira ya hadhira na wahusika, kuzaliwa, kukua na kufa* na *kurithishwa kutoka kizazi hadi kizazi*. Kielelezo Na. 4.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili.



4. "fasihi simulizi ni hai" kwa sababu zifuatazo hapa chini.
i) Kwa sababu huhifadhiwa kichwani ndio maana ni hai la
bda mtu akifa ndio nayo inapotea ama inatoweka
Mfano: pale ambapo mtu amehifadhi fasihi simulizi anauweza w
a kukisimulia kizazi chachike na hicho kizazi nacho kitaja kusi
mulia vizazi vyao huko baadae.

ii) Kwa sababu huhifadhiwa kwenye kompyuta ndio maana huk
aa kuwa hai labda kompyuta iharibike kabisa kasi cha kwamba
haiwezi kutengenezeka ndio nayo itakuwa sio hai tena.
Mfano: Mtu akiangalia picha ama movie katika komputa ataiweka ki
chwani ambapo ataweza pia kuhadithia wengine au wote kujionea
kwa macho.

iii) Kwa sababu huhifadhiwa katika kanda za video, ambayo hupe
lekea fasihi simulizi kuwa hai.
Mfano: kanda ikiwekwa katika tivii na watu wakawa wanaanga
lia wanajifunza kitu na fasihi hubaki kuwa hai tu.

iv) Kwa sababu huhifadhiwa katika vinasa sauti.
Mfano: redio ambayo mtu akisikiliza anavuta picha na anajifu
nza kitu hayo badi hii njia pia hupanga fasihi simulizi ku
bakia kuwa hai sikuzote maisha yote.


Kielelezo Na. 4.1: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 4.

Katika Kielelezo Na. 4.1, mtahiniwa alielezea njia za uhifadhi wa kazi za kifasihi kama vile kichwani, kwenye kompyuta, kwenye kanda za video na vinasa sauti kinyume na matakwa ya swali *badala ya* kuthibitisha kauli "fasihi simulizi ni hai" kwa kueleza sifa anuai za fasihi simulizi.

Watahiniwa 80,826 sawa na asilimia 15.48 walikuwa na ufaulu wa wastani katika swali hili kutokana na kushindwa kuthibitisha kwa

usahihi uhai wa fasihi simulizi. Watahiniwa hao walionesha kutokuwa na ulewa wa kutosha kuhusu sifa anuwai za fasihi simulizi, kwani walitoa hoja zisizojitosheleza. Baadhi yao, walitoa hoja sahihi na kushindwa kuthibitisha baadhi ya hoja kwa mifano. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alielezea uhai wa fasihi simulizi unaotokana na *utendekaji unaomhusisha hadhira na fanani*, lakini alitoa mfano wa kazi zinazohifadhiwa katika video ambapo hadhira hashirikishwi moja kwa moja bali huwa mtazamaji tu. Upungufu wa mifano hiyo ulisababisha kundi hili kupata alama za wastani 1.5 hadi 2.5.

Aidha, watahiniwa wengine, (43,129) sawa na asilimia 8.26 walijibu swali hili vizuri kutokana na kuwa na uelewa mkubwa kuhusu sifa kuu za fasihi simulizi. Kwa ujumla, watahiniwa hao waliweza kutoa hoja sahihi zinazothibitisha uhai wa fasihi simulizi kama vile; *kuwepo kwa utendekaji kati ya hadhira na fanani, kuonana ana kwa ana kati ya hadhira na fanani, kubadilika kulingana na mazingira ya hadhira na wahusika, kuzaliwa, kukua na kufa* na *kurithishwa kutoka kizazi hadi kizazi*. Hivyo, watahiniwa hao waliweza kutoa mfano unaothibitisha kauli "fasihi simulizi ni hai." Kielelezo Na. 4.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa wa aina hiyo.


04 i) Ina hali ya utendaji
mfano: Hadhira hushiriki kwa kupiga makofi pia fanani huo nyimbo na vitendo
ii) Hukutanisha fanani na hadhira ana kwa ana.
mfano: wakati wa uwasilishaji fanani na hadhira hukutana na kuonana na hata kuweza na uwezo wa kuwasiliana ana kwa ana.
04 iii) Fasihi simulizi hubadilika kwenda na mazingira na hupo kwa mabadiliko
mfano: Endapo fanani amekosea ana uwezo wa kuomba radhi na kubadilisha au kurekebisha kwa alicholipanya.
iv) Fasihi simulizi huzaliwa, hukua, huenea na mwisho hufa.
mfano: Hadithi hutungwa, na baadae huwasilishwa kwa watu na huenea na mwisho hupotea


Kielelezo Na. 4.2**:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 4.

Katika Kielelezo Na. 4.2, mtahiniwa aliweza kueleza kwa usahihi sifa kuu za fasihi simulizi kama vile *kuwa na hali ya utendaji, kukutanisha fanani na hadhira, kubadilika kulingana na mazingira* na *kuzaliwa, kukua na kufa*, hivyo kupata alama za juu.

### 2.2.3 Swali la 5: Mjengo wa Tungo

Swali hili lilitoka katika mada ya *Mjengo wa Tungo* na mada ndogo ya *Ufafanuzi wa Aina za Tungo* na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kubaini aina za tungo na uchanganuzi wa sentensi. Swali lilikuwa na vipengele viwili, ambapo kipengele *(a)* kilimtaka mtahiniwa kubainisha miundo minne ya kirai nomino, kwa kutumia mifano na *(b)* mtahiniwa alitakiwa kuchanganua sentensi alizopewa kwa njia ya jedwali; (i) *Umma unalalamika sana* na (ii) *Simba ni mkali ila chui ndiye zaidi.*

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 522,082 sawa na asilimia 100 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani huu. Takwimu zinaonesha kuwa swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyokuwa na ufaulu wa wastani kwani watahiniwa 205,263 sawa asilimia 39.32 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 5 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.





**Chati Na. 5:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 5*

Katika Chati Na. 5, watahiniwa 316,819 (60.68%) walipata alama hafifu (0 hadi 2), watahiniwa 145,518 (27.87%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 2.5 hadi 5.0 na watahiniwa 59,745 (11.44%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 5.5 hadi 8.

Kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili kilikuwa cha chini kwani idadi kubwa ya watahiniwa (60.68%) walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kutokana na kushindwa kubainisha miundo minne ya kirai nomino katika kipengele (a) na kushindwa kuchanganua sentensi walizopewa katika kipengele (b). Ufaulu wa chini wa watahiniwa (39.32%) waliopata 0 ulitokana na kukosa umahiri katika mjengo wa tungo hususani uelewa wa miundo ya virai nomino katika kipengele (a), hivyo kushindwa kuorodhesha miundo hiyo kwa usahihi. Badala yake, walibainisha miundo isiyo sahihi kama vile: *kirai nomino huundwa na shamirisho*; *kirai nomino huundwa na kitenzi kikuu*; *kirai nomino huundwa na kitenzi kisaidizi*; na *kirai huundwa na kivumishi*. Muundo wa pili na wa tatu umetokana na watahiniwa hao kushindwa kuelewa kuwa kirai nomino kinakaliwa na nomino na maneno mengine yanayotoa maelezo juu ya nomino na si kitenzi kwani kitenzi huhusika na kitendo badala ya jina. Katika kipengele (b) walichanganua sentensi kwa kutumia njia ya matawi *badala ya* kuchanganua sentensi zote mbili walizopewa kwa njia ya jedwali kama swali lilivyotaka.

Kutokana na kukosa umahiri kuhusu mjengo wa tungo, baadhi ya watahiniwa katika kipengele (a) walibainisha miundo ya kirai nomino kama *muundo wa kimapokeo*, *muundo wa kisarufi*, *muundo msago* na *muundo wa moja kwa moja;* miundo ambayo inahusika katika utunzi wa kazi za kifasihi kinyume na matakwa ya swali. Watahiniwa walitakiwa kubainisha miundo minne ya kirai nomino kama vile nomino peke yake, nomino zaidi ya moja, nomino na kivumishi, nomino na kishazi tegemezi, kiwakilishi na kivumishi na kiwakilishi peke yake. Pia Katika kipengele (b), watahiniwa walichanganua sentensi walizopewa kwa njia zisizoeleweka na kupata 0. Kielelezo Na. 5.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili.





Kielelezo Na. 5.1: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 5.

Katika Kielelezo Na. 5.1, mtahiniwa alibainisha *shamirisho, kiima, chagizo* na *kivumishi* katika kipengele (a) na kuchora jedwali lililolenga kuchanganua sentensi ya (ii) *Simba ni mkali ila chui ndiye zaidi* ambapo uchanganuzi wake haukueleweka, hatimaye kupata 0.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 145,518 sawa na asilimia 27.87 waliweza kubainisha baadhi ya miundo ya kirai nomino kwa usahihi na kushindwa mingine kutokana na kukosa uelewa stahiki kuhusu miundo ya virai kwa ujumla, hivyo kupata alama za wastani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kubainisha miundo ya kirai nomino katika kipengele (a) lakini alichanganua sentensi zote mbili kwa njia ya matawi kinyume na matakwa ya swali, hivyo akapata ufaulu wa wastani.

Hata hivyo, watahiniwa wachache (59,745) sawa na asilimia 11.44 ndio walioweza kubaini kwa usahihi miundo ya kirai nomino katika kipengele (a) na kuchanganua sentensi kwa njia ya matawi kwa usahihi katika kipengele (b) kama ilivyotakiwa na kupata alama za

juu. Kielelezo Na. 5.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.


5. a) i Muundo wenye nomino moja tu.
Kwa Mfano:
Baba / anakula chakula
KN
ii Muundo wenye nomino mbili na zaidi.
Kwa Mfano:
Asha na Juma / wanalima vizuri
KN
iii Muundo wenye nomino na kivumishi
Kwa mfano:
Mwanafunzi mrefu / ameanguka vibaya.
KN
iv Muundo wenye nomino na kishazi tegemezi vumishi (BV)
Kwa mfano:
Mwanafunzi aliyetoroka / ameadhibiwa.
KN.
5. b) Kuchanganua sentensi "Umma unalalamika sana"
kwa njia ya jedwali.
i)

| S. Sahili | | |
|---|---|---|
| K | A | |
| KN | KT | KE |
| N | T | E |
| Umma | Unalalamika | Sana. |

Kielelezo Na. 5.2: Sehemu ya majibu sahihi katika swali la 5.


Katika Kielelezo Na. 5.2, mtahiniwa alibainisha miundo minne ya kirai nomino katika kipengele (a) na kuchanganua sentensi alizopewa katika kipengele (b) kwa usahihi, akapata alama za juu.

### 2.2.4 Swali la 6: Fasihi Simulizi

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Simulizi*, mada ndogo ya *Ufafanuzi wa Vipera vya Tanzu za Fasihi Simulizi*. Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kutofautisha tanzu na vipera vya fasihi simulizi. Swali liliuliza;

> *Wanafunzi wengi wa Kidato cha Kwanza huchanganya maana za tanzu na vipera vya fasihi simulizi. Ili kuwaondolea mkanganyiko huo, onesha tofauti iliyopo kwa kila seti (a) – (d) kwa kutoa maelezo mafupi na mfano kwa kila moja.*
> *(a) Ushairi na mashairi*
> *(b) Maigizo na vichekesho*
> *(c) Semi na Misemo*
> *(d) Hadithi na visasili*

Watahiniwa 522,082 sawa na asilimia 100 waliofanya mtihani walijibu swali hili. Swali hili lilikuwa na kiwango cha chini zaidi cha ufaulu kati ya maswali yote ya mtihani huu kwani, asilimia 21.47 pekee ndio waliofaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 6 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.





**Chati Na. 6:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 6*

Katika Chati Na. 6, watahiniwa 409,967 (78.53%) walipata alama hafifu (0 hadi 2), watahiniwa 80,975 (15.51%) walifaulu kwa

kiwango cha wastani kwa kupata alama 2.5 hadi 5.0 na watahiniwa 31,140 (5.96%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 5.5 hadi 8.

Watahiniwa wengi (78.53%) waliokuwa na ufaulu hafifu walionesha kukosa umahiri katika kutofautisha tanzu na vipera vya fasihi simulizi. Aidha, zaidi ya nusu ya watahiniwa (59.9%) walipata 0 kwa kushindwa kabisa kuonesha uelewa wa tanzu ama vipera vya fasihi simulizi kwa ujumla, hivyo kushindwa kutofautisha tanzu na vipera vilivyopo katika seti (a) hadi (d). Kutokana na kukosa umahiri huo, baadhi yao walitoa maelezo ya jumla ya tanzu na vipera walivyopewa kwenye kila kipengele husika badala ya kuonesha tofauti iliyopo kati ya tanzu na vipera hivyo. Wengine walielezea tanzu na vipera hivyo kisarufi, hivyo kubainisha aina za maneno kwa kila seti kinyume na matakwa ya swali hili. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika seti (a) alibainisha “ushairi” kama *nomino* na “mashairi” kama *kivumishi*. Kielelezo Na. 6.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili.


06. a) Ushairi na mashairi - ni mtu anatunga Shairi ili kuwe za kulisom : mbele ya watu hao.
b) Maigizo na Vichekesho - ni hali ya watu kuweza kutunga kama vile kamchezo
c) Semi na misemo - huzuka na kupotea baada ya muda Flani
d) Hadithi na Visasili - ni hali ya mtu kuweza kuele zea kitu.

Kielelezo Na 6.1**:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 6.


Katika Kielelezo Na. 6.1, mtahiniwa alitoa maelezo yasiyo na uhusiano wowote na tanzu au vipera alivyopewa kwa kila seti kinyume na matakwa ya swali na akapata alama 0.

Licha ya ufaulu hafifu wa watahiniwa katika swali hili, watahiniwa wachache (15.51%) waliweza kutofautisha baadhi ya seti za tanzu na vipera vya fasihi simulizi walivyopewa, hivyo

kupata alama za wastani (2.5 – 5). Baadhi yao walishindwa kutoa mifano sahihi ili kufafanua tofauti hizo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza tofauti kati ya maigizo na vichekesho katika seti (b) kwa usahihi kwa kuandika *maigizo ni utanzu wenye mpangilio wa maneno unaoambatana na utendaji wa wahusika* na *vichekesho ni mpangilio wa maneno ulio na utendekaji ili kufikisha ujumbe kwa njia ya kuchekesha*; lakini mtahiniwa huyo alishindwa kuonesha tofauti kati ya dhana hizo ambapo vichekesho ni kipera cha maigizo. Pia, alitakiwa kuorodhesha vipera vya utanzu wa maigizo kama vile *michezo ya kuigiza, vichekesho, majigambo, ngonjera, miviga* na *ngoma* ili kuonesha uhusiano uliopo kati ya dhana hizo.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache (31,140) sawa na asilimia 5.96 ya watahiniwa wote waliojibu swali hili walifaulu vizuri kwa kupata alama za juu (5.5 – 8). Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu tanzu na vipera vya fasihi simulizi, hivyo walitumia umahiri huo kutofautisha tanzu na vipera katika seti (a) hadi (d) kwa usahihi. Baadhi ya majibu sahihi ya watahiniwa hao yalikuwa; (a) *Ushairi ni utanzu wenye tungo zenye mpangilio maalum wa silabi, maneno na sentensi unaojumuisha mashairi, tenzi, nyimbo, maghani na ngonjera* wakati *mashairi ni kipera cha ushairi chenye tungo zenye mpangilio maalum wa silabi, uteuzi mahsusi wa maneno, na lugha ya mkato.* (b) *Maigizo ni utanzu wenye mpangilio wa maneno unaoambatana na utendaji wa wahusika* na *vichekesho ni kipera cha maigizo chenye mpangilio wa maneno ulio na utendaji wenye kufikisha ujumbe kwa njia ya kuchekesha;* (c) *semi ni utanzu wenye tungo fupi za kisanaa zitumiazo picha, ishara, na tamathali* ambapo *misemo ni kipera cha semi chenye mafungu ya maneno yanayotumiwa na jamii kwa namna maalum ili kutoa maana inayoafiki ukweli fulani ;* na (d) *hadithi ni utanzu unaohusu masimulizi yenye lugha ya mjazo (nathari)* wakati *visasili ni kipera cha hadithi ambacho hujumuisha hadithi fupi zinazotumia wahusika wa aina mbalimbali wakiwemo miungu na binadamu.* Kielelezo Na. 6.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeeleza

kwa usahihi tofauti kati ya tanzu na vipera vya fasihi simulizi katika seti (a) hadi (d) kwa usahihi.



6. Tofauti za tanzu na vipera ni kama ifuatavyo;

a/ Ushairi ni utanzu wa fasihi simulizi unaohusisha mtiririko wa maneno au mawazo yanayofuata mnwala na mapigo ya sauti. Mashairi, ni kipera cha ushairi kinachoonesha mfuatano na mpangilio wa sauti unaofuata urari wa vina na mizani. Mfano, Mashairi ya chekacheka.

b/ Maigizo ni utanzu wa fasihi simulizi unaotumia sauti na vitendo kutoa ujumbe kwa hadhira. Maigizo pia huitwa sanaa za maonesho, mfano, maonesho ya filamu. Vichekesho ni kipera cha maigizo kinachohusisha vitendo vya mzaha vinavyofurahisha na kuamsha hisia za vicheko kwa hadhira.

c/ Semi ni utanzu wa fasihi simulizi unaohusisha matumizi ya lugha ya kisanaa kwa ufupi na hutumia lugha ya picha kufikisha ujumbe. Misemo ni kipera cha semi kinachotumia lugha ya picha na ni vifungu vifupi vya maneno vyenye lugha ya sanaa na tamathali za semi. Mfano, Mungu si Athuman

d/ Hadithi nia utanzu wa fasihi simulizi unaohusisha masimulizi marefu yanayofanywa na wahusika tofauti waliohusika katika visa tofauti. Visasili ni kipera cha hadithi kinachosimulia visa tofauti vilivyofanywa na wahusika kama vile miungu na binadamu.

Kielelezo Na 6.2**:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 6.

Katika Kielelezo Na 6.2, mtahiniwa alitofautisha kwa usahihi tanzu na vipera vya fasihi simulizi katika seti zote na kupata alama za juu.

### 2.2.5 Swali la 7: Maendeleo ya Kiswahili

Swali hili lilitoka katika mada ya *Kukua na Kuenea kwa Kiswahili baada ya Uhuru* na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kupendekeza namna anavyoweza kukuza na kueneza Kiswahili kwa wageni kwa kutumia (i) *biashara, (ii) utawala, (iii) utamaduni* na *(iv) mafunzo* pamoja na kutoa mfano kwa kila moja.

Watahiniwa 522,082 sawa na asilimia 100 walijibu swali hili. Swali hili lilikuwa na ufaulu wa wastani ambapo watahiniwa 241,422 sawa na asilimia 46.24 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Jedwali Na. 2 linaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.


**Jedwali Na. 2: Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa**

| Alama | Idadi ya Watahiniwa | Asilimia ya Watahiniwa |
|---|---|---|
| 0.0 - 2.0 | 280,660 | 53.76 |
| 2.5 - 5.0 | 191,551 | 36.69 |
| 5.5 - 8 | 49,871 | 9.55 |

Katika Jedwali Na. 2, watahiniwa 280,660 (53.76%) walipata alama hafifu (0 hadi 2), watahiniwa 191,551 (36.69%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 2.5 hadi 5.0 na watahiniwa 49,871 (9.55%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 5.5 hadi 8.

Zaidi ya nusu ya watahiniwa (53.76%) walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kutokana na kukosa umahiri katika mada ndogo ya *Kukua na Kuenea kwa Kiswahili baada ya Uhuru*. Kati yao, watahiniwa 208,662 sawa na asilimia 40 walishindwa kupendekeza namna hata moja watakayotumia ili kukuza na kueneza Kiswahili kwa wageni kupitia (i) biashara, (ii) utawala, (iii) utamaduni, na (iv) mafunzo. Kutokana na kukosa umahiri huo, baadhi ya watahiniwa walitoa mapendekezo yasiyo sahihi katika kukuza na kueneza Kiswahili kupitia vipengele hivyo na

wengine hawakutoa jibu lolote katika swali hili. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alipendekeza katika kipengele cha (i) biashara – *biashara ya watumwa ikomeshwe,* (ii) utawala – *waafrika watawaliwe*, (iii) utamaduni – *utamaduni wa kigeni uenziwe* na (iv) mafunzo – *vijana wafunzwe mambo mbalimbali ya kidunia mfano, uvutaji wa bangi, ushoga na wizi ili kuyaepuka*. Majibu haya yanaonesha kuwa mtahiniwa huyo hakuelewa kuwa swali lilimtaka apendekeze namna atakavyotumia vipengele (i) hadi (iv) katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili kwa wageni kama vile (i) *kuanzisha biashara ya kutengeneza vitu mbalimbali*; (ii) *kuhimiza matumizi ya Kiswahili katika shughuli zote zinazohusu utawala*; (iii) *kuandaa na kuwaalika wageni kushiriki shughuli mbalimbali za kiutamaduni*; na (iv) *kuandaa mpango wa mafunzo kwa wageni kujifunza lugha ya Kiswahili kulingana na mahitaji yao kwa kutumia mbinu anuai za kufunza lugha kwa wageni.* Kielelezo Na. 7.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili.


07 (i) Biashara; biashara za madini
mfano; dhahabu, almasi,
(ii) Utawala;
mfano; Mahakama, bunge
(iii) Utamaduni; Kuhamasisha watu.
Mfano; Upendo, upole, nidhamu
(iv) Mafunzo; katika kuwafunzo mambo
mbali mbali ya dunia
Mfano; Juhudi Umakini Usikivu.

Kielelezo Na 7.1**:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 7.

Katika Kielelezo Na. 7.1, mtahiniwa alieleza mambo yanayohusika katika vipengele (i) biashara, (ii) utawala, (iii)

utamaduni, na (iv) mafunzo, lakini alishindwa kupendekeza namna mambo hayo yatakavyotumika katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili kwa wageni, hivyo akapata 0.

Aidha, watahiniwa 191,551 sawa na asilimia 36.69 ya waliojibu swali hili, walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama kuanzia 2.5 hadi 5. Watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kutosha katika kupendekeza namna watakavyotumia (i) biashara (ii) utawala, (iii) utamaduni, na (iv) mafunzo katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili kwa wageni. Baadhi ya watahiniwa hao walitoa mapendekezo sahihi kwa baadhi ya vipengele lakini wakashindwa kufanya hivyo katika vipengele vingine. Wengine walipendekeza namna watakavyotumia biashara, utawala, utamaduni na mafunzo kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili kwa wageni lakini maelezo yao hayakukidhi matakwa ya swali hili, hivyo kupata alama za wastani.

Watahiniwa wachache sana (49,871) sawa na asilimia 9.55 walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu wa alama kuanzia 5.5 hadi 8. Watahiniwa hao walionesha kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada ya *Maendeleo ya Kiswahili* na mada ndogo ya *Kukua na Kuenea kwa Kiswahili baada ya Uhuru*. Watahiniwa hao walipendekeza kwa usahihi namna watakavyokuza na kueneza lugha ya Kiswahili kwa wageni katika vipengele (i) biashara, (ii) utawala, (iii) utamaduni, na (iv) mafunzo. Majibu sahihi ya watahiniwa hao yalikuwa: (i) Biashara: - kuanzisha biashara ya kutengeneza vitu mbalimbali kama vile fulana, kanga, vikoi na vinyago vyenye maneno ya lugha ya Kiswahili; (ii)Utawala: - kuhimiza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shughuli zote zinazohusu utawala. Kwa mfano, hati za kusafiria na pasi ziandikwe kwa lugha ya Kiswahili; (iii) Utamaduni:- kuandaa na kuwaalika wageni ili washiriki shughuli mbalimbali za kiutamaduni kama; nyimbo, ngoma, mashairi yaliyoandaliwa kwa lugha ya Kiswahili; na (iv) Mafunzo:- kuandaa mpango wa mafunzo ya lugha ya Kiswahili kwa wageni kulingana na mahitaji yao kwa kutumia mbinu anuwai za kufunza lugha kwa wageni. Kwa ujumla, watahiniwa hao walionesha kuwa na umahiri katika

kupendekeza namna watakavyotumia vipengele hivyo katika kukuza na kueneza Kiswahili kwa wageni na kutoa mifano sahihi kwa kila kipengele na kupata alama za juu. Kielelezo Na. 7.2 ni sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa aliyekidhi matakwa ya swali.

7. (i) Biashara

Nitakuza na kueneza Lugha ya Kiswahili kwa wageni kwa kuwahimiza waweze kutumia kiswahili katika kufanya biashara zao. Mfano wa biashara hizo ni kuuza na kununua bidhaa mbalimbali kama vile pamba na mahindi, biashara ya usafirishaji wa bidhaa ndani na nje ya nchi.

ii) utawala

Nitakuza na kueneza Lugha ya Kiswahili kwa wageni kwa kuzingatia kuwa shughuli zote za utalii zinafanyika kwa kiswahili, kwa mfano shughuli za kupokea watalii wanaotoka ndani na nje ya nchi zinapaswa kufanyika kwa kiswahili. pia nitawahimiza wageni wasikipuuze kiswahili.

iii) utamaduni

Nitakuza na kueneza Lugha ya kiswahili kwa wageni kwa kuwaonyesha jinsi tamaduni za kiafrika zinavyo-fanywa kwa kiswahili. Mfano Nitawaonyesha jinsi jamii za kiafrika wanavyofanya shughuli zao za kiutamaduni kama vile Mazishi na Harusi kwa kiswahili.

iv) Mafunzo

Nitakuza na kueneza Lugha ya kiswahili kwa kuwapa mafunzo mbalimbali kwa kutumia Lugha ya kiswahili. Mfano: Nitawapatia mafunzo juu ya njia za kuweza kujikinga na wanyama wakali kama vile simba na chui, pia nitawapa mafunzo juu ya utamaduni wa afrika unavyokuzwa kwa kutumia kiswahili.

Kielelezo Na. 7.2: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 7.

Kielelezo Na. 7.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyependekeza kwa usahihi namna atakavyokuza na kueneza lugha ya Kiswahili kwa wageni katika vipengele (i) *biashara*, (ii) *utawala*, (iii) *utamaduni*, na (iv) *mafunzo* na kupata alama za juu za swali hili.


### 2.2.6 Swali la 8: Ufahamu

Swali hili lilitoka katika mada ya *Ufahamu*, mada ndogo ya *Ufahamu wa Kusoma Kifungu cha Habari* na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kuelewa kifungu cha habari. Swali lilimtaka mtahiniwa kusoma kifungu cha habari kisha kujibu maswali yanayofuata. Kifuatacho ni kifungu cha habari walichopewa.

> *Teknolojia ya habari na mawasiliano hutumiwa kwa lengo la kurahisisha utendaji kazi; kuimarisha ufundishaji; uwazi na kuongeza ufanisi. TEKNOHAMA imetambuliwa na wadau wa elimu kuwa ni muhimu katika shughuli za ufundishaji na ujifunzaji. Lengo la kutumia TEKNOHAMA ni kiurahisisha ufundishaji kwa sababu hudhihirishwa katika hali halisi kwa kutumia aina mbalimbali za TEKNOHAMA.*
>
> *Dunia ya sasa imebadilika; na mambo ya kijamii na kiuchumi yanategemea sana mitandao ya kompyuta. Katika kipindi cha miongo mitano iliyopita mpaka sasa, matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano yamezidi kuenea katika elimu kote ulimwenguni.*
>
> *Ili kufanikisha ufundishaji wa mada mbalimbali, mwalimu anahitaji kutumia TEKNOHAMA kwa ajili ya kupata taarifa na habari kutoka vyanzo mbalimbali, kuendeleza ujifunzaji unaompa mwanafunzi nafasi ya kati na kumpa mwalimu jukumu la kuwa mlezi na mwenezi badala ya ule wa mjua vyote. Mwalimu wa karne hii anaweza kujihusisha na matumizi ya TEKNOHAMA katika ufundishaji wake darasani, hali inayoweza kumpa haueni katika kazi yake.*

*Hata hivyo, katika nchi zinazoendelea walimu wengi hawatumii TEKNOHAMA katika ufundishaji. Hii inatokana na teknolojia hii kuhitaji muda, fedha na maarifa ya ziada kwa watumiaji. Hayo kwa ujumla yanakwamisha utumiaji wa teknolojia hiyo katika elimu. Hivyo, hatuna budi kuhakikisha tunakabiliana na mambo hayo ili kuhakikisha teknolojia hiyo inatumika katika elimu ili kurahisisha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.*

Swali lilikuwa na vipengele viwili (a) na (b). Kipengele (a) kilimtaka mtahiniwa kubainisha matumizi manne ya TEKNOHAMA katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kulingana na kifungu cha habari; na kipengele (b) kilimtaka kufupisha habari hiyo kwa maneno yasiyopungua 60 na yasiyozidi 70. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa ni wa juu zaidi kuliko maswali yote ya mtihani huu kwani watahiniwa 457,546 sawa na asilimia 87.64 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 7 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.





**Chati Na. 7:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 8*

Katika Chati Na. 7, watahiniwa 64,536 (12.36%) walipata alama hafifu (0 hadi 2), watahiniwa 198,947 (38.11%) walifaulu kwa

kiwango cha wastani kwa kupata alama 2.5 hadi 5.0 na watahiniwa 258,599 (49.53%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 5.5 hadi 8.

Katika kujibu swali hili, karibu nusu ya watahiniwa (49.53%) waliweza kubainisha matumizi manne ya TEKNOHAMA katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kama vile; chanzo cha maarifa mbalimbali, kumfanya mwanafunzi kuwa mjuzi wa mambo mbalimbali, kurahisisha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji na kumfanya mwalimu kuondokana na adha mbalimbali/uchovu katika ufundishaji; majibu ambayo yanakidhi kipengele (a). Katika kipengele (b), watahiniwa hao waliweza kufupisha kifungu cha habari kwa kuzingatia taratibu sahihi za ufupisho kama vile: kutumia maneno yao wenyewe bila kupoteza maana ya msingi, idadi sahihi ya maneno (60 – 70), mtiririko wa mawazo wenye mantiki na kuzingatia taratibu za uandishi; hivyo kupata alama za juu katika swali hili. Kielelezo Na. 8.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu maswali yaliyotokana na kifungu cha habari (ufahamu) kwa usahihi.



8 (a) Matumizi manne ya TEKNOHAMA.

(i) Kurahisisha utendaji wa kazi
(ii) Kuimarisha ufundishaji
(iii) Uwazi
(iv) Kuongeza ufanisi.


(b) Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA) hutumiwa kwa lengo la kurahisisha utendaji kazi, kuimari sha ufundishaji, uwazi na kuongeza ufanisi njia hii imewasaidia sana walimu katika njia ya ufundishaji. Hata hivyo katika nchi zinazoendelea walimu wengi hawatumii (TEKNOHAMA) kwa sababu inahitaji muda, fedha na maarifa ya ziada kwa watumiaji na hivi vyote vinakwamisha utumiaji wa teknolojia huyo katika elimu, hivyo ni lazima tukabiliane na mambo hayo ili kuhakikisha teknolojia hiyo inatumika katika elimu.

Kielelezo Na. 8.1: Majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali la 8.

Katika Kielelezo Na. 8.1, mtahiniwa alionesha kuwa na uelewa wa kifungu cha habari na kujibu vipengele (a) na (b) kwa usahihi na kupata alama za juu. Aidha, mtahiniwa huyo hakutoa ufafanuzi unaotosheleza matumizi ya TEKNOHAMA kama ilivyotakiwa isipokuwa kwa kutaja pekee.

Watahiniwa 198,947 (38.11%) walijibu swali hili na kupata alama za wastani (2.5-5) kutokana na kutoa majibu yasiyojitosheleza kwa baadhi ya vipengele, hususani kipengele (b). Kipengele hiki kilionekana kuwa na changamoto kwa baadhi ya watahiniwa katika kundi hili kwani wengi wao walinakili kifungu cha habari moja kwa moja bila kutumia maneno yao wenyewe na kuandika ufupisho usiokidhi vigezo na kupata alama za wastani.

Hata hivyo, watahiniwa wachache (64,536) sawa na asilimia 12.36 ya watahiniwa waliojibu swali hili walionesha kukosa umahiri wa kusoma kwa ufahamu kisha kujibu maswali yanayotokana na kifungu hicho. Aidha, watahiniwa hao walikosa maarifa kuhusu matumizi ya TEKNOHAMA kama yalivyofafanuliwa kwenye habari kama vile *chanzo cha maarifa mbalimbali*; (ii) *kumfanya mwanafunzi kuwa mjuzi wa mambo mbalimbali*; (iii) *kurahisisha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji*, na (iv) *kumfanya mwalimu kuondokana na adha mbalimbali/uchovu.* Katika kipengele (b), watahiniwa hao walishindwa kufupisha kifungu cha habari kwa maneno yasiyopungua 60 na yasiyozidi 70, kuandika ufupisho usiozingatia maneno yake mwenyewe bila kupoteza maana ya msingi; idadi ya maneno; mtiririko wa mawazo wenye mantiki; na taratibu za uandishi. Kielelezo Na. 8.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu vipengele vyote vya swali hili na kupata 0.


8 (a) i) Kukuza Teknologia yetu ya nchi
ii) Nchi yetu iweze kuendelea mbele.
iii) Nchi yetu iweze kukua kisayansi na teknologia
iv) ili tuepuke na magonjwa kwa kutumia chokaa kufundishia au chaki
(b) TEKNOHAMA NIVEMA IKATEIWA KATIKA NCHI YETU YA TANZANIA ILI KUEPUKA MAGONJWA YA WALIMU KUFUNDISHA NA CHAKI HATA IVO VILEVILE NCHI YETU ITAKUWA KWA KIWANGO KIKUBWA SANA

Kielelezo Na. 8.2: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 8.

Katika Kielelezo Na. 8.2, mtahiniwa alitoa majibu yasiyozingatia matakwa ya swali katika vipengele vyote kwa kuandika matumizi

ya TEKNOHAMA yasiyohusiana na habari katika kipengele (a) na kuandika ufupisho usiokidhi matakwa ya swali na kwa herufi kubwa katika kipengele (b).

## 2.3 SEHEMU C: MASWALI YA MAJIBU MAREFU


Sehemu C ilikuwa na maswali manne ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali matatu. Kila swali lilikuwa na alama 15, hivyo kufanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama 45.

### 2.3.1 Swali la 9: Uandishi wa Insha

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uandishi*, mada ndogo ya *Uandishi wa Insha za Hoja* na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kuunda dhana/mawazo mbalimbali ili kutetea hoja na kufikisha ujumbe fulani. Swali lilimtaka mtahiniwa kuandika insha yenye maneno yasiyopungua mia mbili (200) na yasiyozidi mia mbili na hamsini (250) kuhusu “Manufaa ya Sayansi na Teknolojia kwa Maendeleo ya Kiswahili.” Swali liliuliza;

> *Chama cha Waandishi wa Vitabu Tanzania kimeanzisha shindano la uandishi wa insha kuhusu Manufaa ya Sayansi na Teknolojia kwa Maendeleo ya Kiswahili. Ukiwa miongoni mwa wanachama, andika insha isiyopungua maneno mia mbili (200) na isiyozidi maneno mia mbili na hamsini (250) kuhusu shindano hilo.*

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 298,773 sawa na asilimia 57.23 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vibaya na idadi kubwa ya watahiniwa. Kiwango cha ufaulu kilikuwa cha wastani kwani watahiniwa 106,503 tu sawa na asilimia 35.65 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 8 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.





**Chati Na. 8:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 9*

Katika Chati Na. 8, watahiniwa 192,270 (64.35%) walipata alama hafifu (0 hadi 4), watahiniwa 84,335 (28.23%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 4.5 hadi 9.5 na watahiniwa 22,168 (7.42%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 10 hadi 15.

Takwimu zinaonesha kuwa zaidi ya nusu ya watahiniwa (64.35%) waliojibu swali hili walitoa majibu yasiyokidhi matakwa ya swali na kupata alama hafifu (0 – 4). Watahiniwa hao walishindwa kuandika insha iliyohusu *Manufaa ya Sayansi na Teknolojia kwa Maendeleo ya Kiswahili* yenye maneno kati ya mia mbili (200) hadi mia mbili na hamsini (250). Baadhi yao waliandika insha isiyozingatia vigezo muhimu kama vile kutumia lugha fasaha na sanifu, kuwa na mtiririko na ushikamani wa mawazo, matumizi sahihi ya alama za uandishi na idadi stahiki ya maneno. Wengine waliandika insha bila kuzingatia kiini cha insha. Kwa mfano mtahiniwa mmoja aliandika insha kuhusu *Sayansi na Teknolojia* na kuonesha namna inavyosaidia katika *kuimarisha biashara*; *kujenga ushirikiano*; *kupata taarifa mbalimbali*; *kutengeneza bidhaa mbalimbali* na *kuboresha miundo mbinu*. Majibu haya yalikuwa kinyume na matakwa ya swali hili kwani mtahiniwa alitakiwa kueleza faida za *Sayansi na Teknolojia kwa Maendeleo ya Kiswahili* kama vile kuzuka kwa maneno mapya ya Kiswahili;

kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili katika nyanja za elimu, uchumi na siasa; kuenea kwa utamaduni wa Kiswahili ndani na nje ya nchi (kupitia ongezeko la wasanii wanaoimba kwa Kiswahili kisha nyimbo zao kuwekwa kwenye mtandao); kuongezeka kwa wataalamu mbalimbali wa mifumo ya kikompyuta ya lugha ya Kiswahili na kuongezeka kwa wageni wanaojifunza lugha ya Kiswahili. Kielelezo Na. 9.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili na kupata alama hafifu.


9 Sayansi na Teknolojia: Hukuza maendeleo au uchumi wa inchi ~~isiyo~~ ya tanzania kwa kukuza sayansi na teknolojia inapatikana tanzania na point zifuatazo ni.

Husaidia katika kuendeleza ujuzi: hii husaidia katika jamii kuhuna kufanya katika jamii au ... yako kukuza na kuendeleza kwa kufanya kazi kama kuendeleza. Ujuzi wa viwanda.

Hupeleka maendeleo ya viwanda: Hii hutokea pale ambapo viwanda vinavyopatikana tanzania vina weza kusaidia maendeleo ya kiuchumi katika inchi yako na wananchi waliopo Tanzania.

Kukuza sekta ya uchimbaji wa madini: Hii hutokea pale ambapo miladi mingi au migodini mingi inapopatikana tanzania ina saidia kukuza uchumi kwa kupitia sekta ya uchimbaji madini ya Tanzania.

Kuongeza uzalishaji mali: Hii hupatikana pale ambapo mali za kitanzania zinapo endelea kuzalisha mali tanzania inapatikana sana sana Tanzania

Kielelezo Na. 9.1: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 9.

Katika Kielelezo Na. 9.1, mtahiniwa aliandika faida za sayansi na teknolojia kwa maendeleo ya uchumi wa nchi ya Tanzania kama vile *kuendeleza ujuzi, kupeleka maendeleo ya viwanda, kukuza sekta ya uchimbaji madini* na *kuongeza uzalishaji mali* kinyume na matakwa ya swali.

Watahiniwa 84,335 (28.23%) waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango cha wastani kutokana na kutoeleza hoja madhubuti na za kutosha kwenye nsha juu ya *Manufaa ya Sayansi na Teknolojia kwa Maendeleo ya Kiswahili*. Baadhi yao, walirudia hoja moja zaidi ya mara mbili, jambo lililowafanya kupata alama pungufu kwa hoja hizo. Pia wengine hawakuandika kichwa cha insha; kuandika utangulizi usiokidhi vigezo; kuandika bila kuzingatia alama za uandishi kama vile matumizi ya alama ya mkato na kituo; na walioandika hitimisho lisiloendana na hoja zilizojadiliwa katika insha husika. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa walichanganya hoja kwa kuelezea *mchango wa sayansi na teknolojia katika maendeleo ya Kiswahili* na *maendeleo ya Kiswahili katika kukuza uchumi*; majibu ambayo hajitoshelezi kulingana na matakwa ya swali, hivyo kupata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache (22,168) sawa na asilimia 7.42 walijibu vizuri swali hili kwani walionesha kuwa na uelewa wa kutosha juu ya uandishi wa insha za hoja. Watahiniwa hao waliweza kutathmini kwa usahihi *manufaa ya sayansi na teknolojia kwa maendeleo ya Kiswahili* kwa kuandika *utangulizi* mzuri na kutoa maelezo toshelevu kwenye kiini cha insha, kueleza hoja madhubuti zenye mifano mbalimbali kuhusu faida za sayansi na teknolojia kwa maendeleo ya Kiswahili kama vile; *kuzuka kwa maneno mapya ya Kiswahili, kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili katika elimu, uchumi na siasa, kuenea kwa utamaduni wa Kiswahili ndani na nje ya nchi* (*kupitia ongezeko la wasanii wanaoimba kwa Kiswahili kisha nyimbo zao kuwekwa kwenye mtandao), kuongezeka kwa wataalamu mbalimbali wa mifumo ya kikompyuta ya lugha ya Kiswahili* pamoja na *kuongezeka kwa wageni wanaojifunza lugha ya Kiswahili*. Pia watahiniwa hao waliweza kutoa *hitimisho* sahihi kulingana na matakwa ya swali. Kielelezo Na. 9.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama za juu.

9. MANUFAA YA SAYANSI NA TEKNOLOGIA KWA MAENDELEO YA KISWAHILI

Sayansi na Teknolojia; Ni sekta ambazo zinahusisha matumizi ya mashine mbalimbali katika kurahisisha kazi mbalimbali katika fani. Mfano matumizi ya simu za Mkononi, majembe ya kisasa. Sayansi na Teknolojia vina manufaa makubwa katika maendeleo ya kiswahili kama inavyooneshwa hapa chini;

Inarahisisha kujifunza lugha ya kiswahili; kwa kupitia Sayansi na teknolojia wanafunzi wengi wa lugha ya kiswahili humtumika katika urahisishaji wa kujifunza lugha hiyo. Mfano Mtu anaweza kujifunza lugha ya Kiswahili kwa kupitia simu janja kwa urahisi.

Inarahisisha katika kutangaza lugha ya kiswahili; Watu wa mataifa mengi wanaweza kujua lugha ya kiswahili kutokana na jinsi mchango wa Sayansi na ~~Tekno~~ Teknolojia unavyopelekea kukua kwa lugha hii ya kiswahili. Mfano Matangazo ya utalii nje ~~ya~~ za Nchi.

Inapelekea kuongezeka kwa watumiaji wa lugha ya kiswahili. Suala hili pia ni muhimu katika maendeleo ya kiswahili kwani hupelekea watumiaji wa lugha ya kiswahili kuongezeka kwa kasi mfano China, Afrika kusini wanajifunza lugha ya kiswahili kwa kasi kutokana na sayansi na Teknolojia kuendelea.

Inapelekea kuongezeka kwa misamiati. Pia sayansi na Teknolojia inapelekea kuongezeka kwa misamiati ya lugha ya kiswahili jambo ambalo huchochea maendeleo ya kiswahili mfano misamiati kama Runinga, Televisheni.

Inaongeza umaarufu wa lugha ya kiswahili; Pia maendeleo ya sayansi na teknolojia yanapelekea kuongeza umaarufu wa lugha ya kiswahili na kufanya ijulikane maeneo tofautitofauti mfano Marekani, Uingereza na uchina.

9. Kwa ujumla; Sayansi na Teknolojia ni muhimu katika kukuza na kueneza lugha ya kiswahili ndani na nje ya nchi hivyo basi ni muhimu kuidumisha ili kupata maendeleo hayo.


Kielelezo Na. 9.2: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 9.

Kielelezo Na. 9.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuandika vizuri insha kuhusu *Manufaa ya Sayansi na Teknolojia kwa Maendeleo ya Kiswahili*, japokuwa insha yake ilikuwa na makosa ya *kisarufi* kama vile kutumia neno *inapelekea* badala ya 'inayosababisha.'

### 2.3.2 Swali la 10: Uhakiki wa Ushairi

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi* katika mada ndogo ya *Uhakiki wa Ushairi* na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kuchambua kazi mbalimbali za kifasihi hususani ushairi. Swali lilimtaka mtahiniwa kuchagua mashairi matatu kwa kila diwani kutoka katika diwani mbili alizosoma kisha aeleze mafunzo yatakayojumuishwa katika shairi atakalotunga na kughani siku ya mahafali ya Kidato cha Nne ili kuwasaidia wahitimu kuboresha maisha yao ya baadaye.

Watahiniwa 270,594 sawa na asilimia 51.83 walilijibu swali hili. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri ambapo watahiniwa 214,081 sawa na asilimia 79.12 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 9 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 9**: *Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 10*

Katika Chati Na. 9, watahiniwa 56,513 (20.88%) walipata alama hafifu (0 hadi 4), watahiniwa 57,140 (21.12%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 4.5 hadi 9.5 na watahiniwa 156,941 (58%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 10 hadi 15.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa wengi (58%) walionesha umahiri katika uhakiki wa ushairi kwani waliweza kuchagua mashairi na kueleza mafunzo sahihi yatayojumuishwa katika shairi lao likaloghaniwa katika mahafali ya Kidato cha Nne ili kuwasaidia wahitimu kuboresha maisha yao ya baadaye. Miongoni mwao, asilimia 2.5 walipata alama zote za swali hili kwani waliweza kueleza mafunzo katika mashairi matatu yaliyochaguliwa katika diwani mbili kwa usahihi. Diwani hizo zilihusisha "Wasakatonge", "Malenga Wapya" na "Mashairi ya Chekacheka." Miongoni mwa hoja walizotoa katika diwani mbalimbali ni kama ifuatavyo:

Katika diwani ya “Wasakatonge” walieleza vizuri mafunzo na kutoa mifano sahihi ya mashairi kwa kila funzo walilolieleza na kukidhi matakwa ya swali kama vile: *athari za tohara kwa wanawake* katika shairi la ‘Tohara’ *tatizo la rushwa* (Kansa) na *ukosefu wa haki ya kujieleza* (Marufuku). Aidha, katika diwani ya “Mashairi ya Chekacheka” walieleza mafunzo kama vile *wasanii kuacha tabia ya woga* (Tuambae Ukasuku); *mapenzi ya dhati* (Penzi Lisilo Heshima) na *matumizi mabaya ya fedha za umma* (Gunia la Mikutano). Pia katika diwani ya “Malenga Wapya” walieleza mafunzo kama vile *Kufanya kazi kwa bidii* (Tuzingatie Haya); *Wanawake waachane na unyonge na wajikomboe* (Kifungo); na *wanajamii kujenga tabia ya kuheshimiana* (Maisha ni kama Njia*)*. Kielelezo Na. 10.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri na kukidhi matakwa ya swali hili.

Mashairi ni mpangilio wa beti zilizobeba ujumbe ndani yake. Katika Mashairi Fanani huweza kutunga mashairi yaliyobeba dhamira ndani yake. Katika mashairi ya WASAKATONGE iliyoandikwa na M.S. KHATIBU pamoja na MALENGA WAPYA iliyoandikwa na TAKILUKI. Yafuatayo ni mafunzo yanayotokana na mashairi hayo kwa kuanza na shairi la WASAKATONGE.

Shairi la Nahodha linawaasa watu kuacha uongozi mbaya. Katika shairi hili mtunzi lengo lake ni kueleza kuhusu mambo yanayofanywa na baadhi ya viongozi na kupelekea matatizo kwa wananchi wao kama anavyosema

"Nahodha
Wanang'ang'ania sukani
Abiria soto, tunatoseka
Tapeka, kulewa na kutapika".

Hivyo basi watu wanashauriwa wakawe viongozi bora katika jamii zao ili kuleta maendeleo.

Shairi la ~~mwana~~ Tohara kwa wanawake linawaasa watu kuacha mila na desturi potofu. Katika shairi hili mwandishi anawaasihi ~~waand~~ wanajamii kuhusu suala la ukeketaji kwa wanawake kwa kupelekea madhara kama anavyosema

Tohara kwa wanawake, ni hatari
Madhara kwa wako uko, huathiri
Hasara ya peke yake, hudhihiri"

Hivyo basi basi wanafunzi wanapaswa wakatokomeza mila hiyo ili kuweza ~~kuto~~ kujenga jamii yenye maendeleo mazuri.

Shairi la wewo jiko la shamba lina waasa watu kuacha tabia mbaya. Katika shairi hili mwandishi ~~tt~~ anawaasa watu kuachana na tabia mbaya kama ulo umalaya kama ~~ne~~ anavyosema katika shairi.

"Wewo jiko la shamba, si kuko si serodani
Mozoea kumbakumba, kila aina ya kuni"

Hivyo basi watu wanapaswa kuwa na mapenzi ya dhati kwa wenzao na sio kubiriki vitondo vibaya na tabia mbaya.

Katika Mashairi ya MALENGA WAPYA yaliyotayo ni mashairi yenye mafunzo ndani yake.

Shairi la puuzo linowaasa viongozi waachane na uongozi mbaya. Katika shairi mwandishi anawasa watu waliokuwa madarakani kuachana na uongozi unaowaumiza wananchi wao kama anavyosema

"Unapokuwa na shida, wao wanokupuuza
Wanajitia kidada, na kujifanya ajiza
Wajifanya hawajali."

Hii inaonesha jinsi ambavyo ~~tt~~ viongozi hawatoi msaada kwa wananchi wao na ~~kuo~~ kuufanya uongozi kuwa wa manufaa yao tu.

Shairi la israfu linawaasa watu kutumia vizuri mali. Shairi hili linaonesha jinsi ambavyo watu wanapaswa kutumia mali yao na si kuiharibu kama anavyosema

"Mali uliyojichumia
Ni yako nakubali
Lakini kiangalia
Ni vipi unaitumia
Nakusihi mwenzangu israfu haifai"


Hivyo basi watu wanapaswa kutumia mali yao vizuri

Kielelezo Na. 10.1: Sehemu ya majibu sahihi katika swali la 10.

Katika Kielelezo Na. 10.1, mtahiniwa alibainisha mashairi ya *Nahodha, jiko la shamba* na *Tohara* katika diwani ya "Wasakatonge" na *Israfu, Puuzo* na *Samaki Mtungoni* kutoka katika diwani ya "Malenga Wapya." Mtahiniwa huyo alitoa hoja sahihi kuhusu mafunzo yanayotokana na mashairi hayo kulingana na matakwa ya swali na kupata alama za juu.

Hata hivyo, asilimia 21.12 ya watahiniwa wengine waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango cha wastani kutokana na kutoa hoja zenye mapungufu au zisizojitosheleza kutoka katika diwani husika. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kueleza mafunzo sahihi kutoka katika diwani ya "Wasakatonge" kama vile; *kuifundisha jamii umuhimu wa kuwa na mapenzi ya dhati* na *athari za tohara kwa wanawake* lakini baadhi ya mifano ya mashairi aliyotoa hayakuwa halisi ambapo alitaja shairi la *Samaki Mtungoni* na *Tuambae Ukasuku* ambayo hayapo katika diwani husika, hivyo kupata alama za wastani.

Baadhi ya watahiniwa (20.88%) waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu hafifu kwani walionesha kukosa umahiri kuhusu dhana nzima ya ushairi na uhakiki wa kazi za fasihi andishi kwa ujumla. Watahiniwa hao walishindwa kuchagua mashairi matatu kutoka katika kila diwani na kueleza mafunzo kwa kila moja kama ilivyotakiwa. Baadhi yao walitaja dhamira mbalimbali zilizomo katika diwani hizo kama vile *rushwa, uhujumu uchumi, uongozi mbaya, mapenzi ya dhati, uzalendo* na *ugumu wa maisha* bila kuhusisha mashairi yenye mafunzo yaliyotolewa na washairi katika diwani husika. Watahiniwa wengine walishindwa kunukuu kwa usahihi mashairi kwa kuchanganya diwani yanamopatikana mashairi hayo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitumia shairi la *Nahodha* linalohusu tabia zisizofaa za viongozi na kuonesha kuwa shairi hilo linapatikana katika diwani ya "Mashairi ya Cheka Cheka" badala ya "Wasakatonge." Kielelezo Na. 10.2 ni sampuli ya sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili.


10 Taswira; Ni lugha ya picha inayowasilishwa kwa njia ya picha naanza na kitabu cha malenga wapya kilicho andikwa na TAKILUKI / DUP
Taswira ya "ua" ua ingelezwa kama msichana mzuri mlembo na anayehitaji matunzo mshairi ana sema
"Rangi yake ya sanaa machoni inamtia
ukiliona la ng'aa moyoni lakuingia
ua sasa limepea macho walikodoka
Taswira ya "punda" punda imeelezwa kama watu wanao nyanyasa tabaka la chini mshairi anasema
"Toka uzaliwe maishani kizigo
hujawahi kuenziwa waishi ilingenyongo
Hakika umeonewa hukusitaili kipigo"
Taswira ya "puuzo" puuzo imeelezwa kama viongozi wanaopenda madalaka kuliko hazi ya binadamu mshairi anasema
"Ofisini ukiingia waowanakupuuza,
Muda uliofika wao hawauthamini
wanakuweka baoni wanakwambia subiri


Kielelezo Na.10.2: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 10.

Kielelezo Na. 10.2 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa ambaye alibainisha *taswira* ya ‘puuzo’ na ‘punda’ katika diwani ya “Malenga Wapya” badala ya kuchagua mashairi na kueleza mafunzo stahiki kwa kila shairi kama ilivyotakiwa.

### 2.3.3 Swali la 11: Uhakiki wa Riwaya

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi,* mada ndogo ya *Uhakiki wa Riwaya* na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kutathmini maandishi ya kifasihi. Swali lilimtaka mtahiniwa kuthibitisha kauli “Matatizo ya mwanajamii huletwa na mwanajamii mwenyewe” katika riwaya mbili alizosoma.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 496,809 sawa na asilimia 95.16 ya wote waliofanya mtihani. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri sana kwani watahiniwa 435,290 sawa na asilimia 87.62 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 10 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 10**: *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 11*

Chati Na. 10 inaonesha kuwa watahiniwa 65,519 (12.38%) walipata alama hafifu (0 hadi 4), watahiniwa 110,408 (22.22%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 4.5 hadi 9.5 na watahiniwa 324,882 (65.39%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama 10 hadi 15.


Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa asilimia 65.39 ya watahiniwa walikuwa na ufaulu wa kiwango cha juu kwa kupata alama kuanzia 10 hadi 15 kutokana na kuonesha kuwa na maarifa ya kutosha katika kuhakiki riwaya. Kati yao, asilimia 9.9 walipata alama za juu zaidi (14 hadi 15) kwa kuwa waliweza kutoa hoja tatu sahihi kwa kila riwaya katika riwaya mbili walizosoma katika kuthibitisha kauli isemayo "Matatizo ya mwanajamii huletwa na mwanajamii mwenyewe." Katika riwaya ya "Joka la Mdimu" walitoa hoja kama vile *rushwa, kutokuwa na mapenzi ya dhati*, *kukosa uzalendo* na *ujangili;* katika riwaya ya "Watoto wa Mama N'tilie" walitoa hoja kama vile *ukosefu wa elimu*, *ulevi, wizi* na *ujambazi* ambapo katika riwaya ya "Takadini" walitoa hoja

kama *ubaguzi*, *mila potofu*, *ndoa katika umri mdogo* na *ndoa za mitala*; matatizo ambayo wanajamii wamejiletea wenyewe katika riwaya husika. Watahiniwa hao walitoa hoja zikiambatana na mifano sahihi kutoka kwenye riwaya hizo ili kuthibitisha usemi huo. Aidha, waliandika utangulizi mzuri wenye ufafanuzi sahihi kuhusu matatizo yaliyopo katika jamii kwa ujumla. Pia waliweza kuandika hitimisho zuri lililokidhi matakwa ya swali. Kielelezo Na. 11.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama za juu.

11. Jamii imekuwa ikikumbwa na matatizo
mbalimbali. Matatizo hayo yamekuwa yakisababishwa
aidha kutokana na mazingira au na wanajamii wenyewe.
Waandishi wa riwaya mbalimbali wamekuwa wakionesha
matatizo ambayo yamekuwa yakiletwa na wanajamii.
Kwa kutumia riwaya ya "WATOTO WA MAMA NTILIE" iliyo-
andikwa na Emmanuel Mbogo pamoja na "TAKADINI"
iliyoandikwa na Ben J. Hanson; yafuatayo ni matatizo
yaliyoletwa na wanajamii. Kwa kuanza na "WATOTO WA
MAMA NTILIE";

Ukosefu wa elimu. Tatizo hili limeweza kuthibi-
tika kwa wahusika Pita, Zita na Musa ambao walifukuzwa
shule na Mwalimu Chikoya kwa kushindwa kulipa ada na
kukosa sare za shule. Hivyo, Mwalimu Chikoya anaonekana
kuwa kisababishi cha ukosefu wa elimu kwa watoto
kama Pita na Zita.

Biashara ya madawa ya kulevya. Biashara
hii ya madawa ya kulevya imeweza kuonekana kwa



11. Mhusika Musa ambaye alikuwa akijihusisha na madawa ya kulevya akimfanyia kazi Masta Baroni. Musa anafanikiwa kumuingiza Pita katika Biashara hiyo pia. Hivyo Masta Baroni anathibitika kuwa mtu anayeleta matatizo kwa kuwaajiri watoto katika Biashara yake haramu.

Umaskini. Tatizo hili la umaskini limeweza pia kuonekana kuwa linasababishwa na wanajimii wenyewe. Hii ni kwa sababu Mzee lomolomo ambaye ni mume wa mama ntilie alikuwa ni mlevi na asiyefanya kazi kwa ajili ya familia yake. Hii inapelekea Mama ntilie kupambana na kuhangaika mwenyewe. lakini pia askari wa jiji waliokuwa wakipokea rushwa kwa Mamantilie waliweza kuunyonya mtaji wote wa Mama ntilie, hivyo kuyafanya maisha yake magumu. Kwa kutumia riwaya ya "TAKADINI";

Magomvi na Migogoro kutokana na mila potofu ya ndoa za mitala. Hii ni kwa sababu mwandishi anathibitisha kuwa ndoa ya mitala ni chanzo cha Mifarakano na migogoro katika familia. Dadirai pamoja na Rumbidzai wanathibitika kuwa na chuki dhidi ya Sekai ambaye alikuwa ni mke mwenza kwa Bwana Makwati. Hii ni baada ya wao kuwa na wivu kwa sekai. Hivyo ndoa za mitala zinazofanywa na wanajamii ni chanzo cha migogoro.

Unyanyapaaji wa walemavu wa ngozi. Tatizo hili limeonekana kwa mhusika Takadini ambaye alikuwa akinyanyaswa na kutengwa na wanajamii, kwa sababu ya ulemavu wa ngozi aliokuwa nao. Watu waliamini kuwa alikuwa ni laana za mababu, hivyo walimtenga na kumnyanyapaa.

Matatizo ya kifamilia. Matatizo haya yamethibitika kupitia Bwana Makwati ambaye anamkataa mwanae kwa kuwa alizaliwa akiwa na ulemavu wa ngozi.

Kielelezo Na.11.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 11.


Katika Kielelezo Na. 11.1, mtahiniwa aliweza kuthibitisha kauli kuwa “matatizo ya mwanajamii huletwa na mwanajamii mwenyewe” katika riwaya ya “Watoto wa Mama N'tilie” na “Takadini” na kupata alama za juu.


Aidha, asilimia 22.22 ya watahiniwa waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kuwa waliweza kuthibitisha kauli kuwa "matatizo ya mwanajamii huletwa na mwanajamii mwenyewe" kwa kuwa baadhi walitoa hoja chache na wengine walitoa hoja zisizojitosheleza kutoka katika riwaya teule. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja, alitoa hoja kuhusu *umaskini* katika riwaya ya "Watoto wa Mama N'tilie" lakini alibainisha chanzo cha tatizo hili kuwa ni kifo cha Mzee Lomolomo badala ya ulevi wake, hivyo kusababisha kupata alama za wastani.

Watahiniwa wachache (61,519) sawa na asilimia 12.38 waliojibu swali hili walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu. Ufaulu huo ulitokana na kukosa umahiri wa kutosha juu ya uhakiki wa kazi za fasihi andishi, hususani riwaya teule. Watahiniwa hao walishindwa kutoa hoja tatu sahihi kwa kila riwaya kati ya riwaya mbili walizosoma ili kuthibitisha usemi usemao "Matatizo ya mwanajamii huletwa na mwanajamii mwenyewe." Badala yake, baadhi walitoa hoja ambazo hazikukidhi matakwa ya swali ambapo miongoni mwao walibainisha matatizo yaliyosababishwa na wanajamii kwenye tamthiliya teule badala ya riwaya. Watahiniwa wengine walibainisha *dhamira, migogoro* na *ujumbe* mbalimbali kutoka riwaya teule bila kutoa uthibitisho wa usemi waliopewa kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza juu ya migogoro iliyojitokeza katika riwaya ya "Takadini" kama vile *mgogoro kati ya Sekai na mume wake Makwati; mgogoro kati ya Shingai na wazazi wake; wanakijiji na Takadini;* na katika riwaya ya 'Watoto wa Mama N'tiliye' alieleza *migogoro kati ya Peter na Dotto; kati ya Mama N'tiliye na serikali;* na *kati ya Mama N'tiliye na Mzee Lomolomo* badala ya kuonesha namna matatizo katika jamii husika yalivyoletwa na mwanajamii wenyewe kama swali lilivyomtaka.

Kwa ujumla watahiniwa hao walitakiwa kuthibitisha kauli isemayo "Matatizo ya mwanajamii huletwa na mwanajamii mwenyewe" kwa kubaini matatizo mbalimbali katika riwaya teule kama vile: "Joka la Mdimu" tatizo la *ujambazi, wizi na ujangili* lililosababishwa na Brown Kwacha kwa kuwa aliwatuma watu

kuwinda wanyamapori bila kibali na kusababisha tatizo la ujangili katika jamii*;* tatizo la *kufanya mapenzi nje ya ndoa/kukosa uaminifu* lililosababishwa na Brown Kwacha, Josephina na Leila. Vilevile, *tatizo la rushwa* lililosababishwa na Brown Kwacha aliyekuwa anapokea rushwa na kusababisha kuwapo kwa tatizo hilo katika jamii yao. Pia katika riwaya ya "Watoto wa Mama N'tilie" walitoa hoja kama vile *ukosefu wa elimu, ulevi, wizi* na *ujambazi* ambapo katika riwaya ya "Takadini" walitoa hoja kama *ubaguzi, mila potofu*, *ndoa katika umri mdogo* na *ndoa za mitala*; matatizo ambayo yalithibitika kuwepo katika jamii na yaliyoletwa na wanajamii wenyewe katika riwaya husika. Kielelezo Na. 11.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili na kupata alama hafifu.


11. Migogoro ; ni kitendo ambacho watu hufanya
na kuleta migogoro baina ya watu wawili au
zaidi. Ni kweli matatizo ya mwanajamii huteruwa na
mwanajamii mwenyewe. kwa kutumia riwaya ya
TAKADINI MWANDISHI BEN. J. HANSON na WATOTO WA
MAMA NTILIE MWANDISHI E. MBOGO Ina thibitika
kama ifuatavyo. Vifuatavyo ni migogoro ambayo
imetokea.
-katika riwaya ya TAKADINI MWANDISHI BEN.
J. HANSON.
Migogoro kati ya Makwati na Sekai ; migogoro
huu ni pale ambapo makwati ana mchukia mtoto
wake kwakuwa ni mtoto zeruzeru na mama
alimkataza kufanya mahusiano naye kuwa ni
aliamini zeruzeru ni mkosi kabisa kwa hiyo
mwanake Takadini ni zeruzeru. ~~net~~ katika jamii
yetu tunaona kuwa baadhi ya watu huwafanya


watoto wao kutengwa na wazazi. Hatu paswi kuwa
hivyo tuwe wakalimu na upendo kwa watu wote.
Migogoro kati ya Sekai na kijiji; tunaona kuwa
Sekai aligombana na kijiji kwa sababu ya mtoto
wake Takadini na maama wanamwita ~~mgogo~~
mgonjwa na ngozi ndo maana wanamtenga
hawataki kukaa na Takadini. Wanakijiji wanataka
Sekai ahame. Katika jamii yetu tunaona kuwa watu
wengi huwa na ubaguzi kwa sababu baadhi ya
watu hutenga watu wenye ulemavu. Hatupaswi kufanya
hivyo.
Migogoro kati ya Takadini na Wanakijiji; hii ni
pale ambapo tunaona kuwa Takadini aligombana na
watu kijijini kwa sababu ya ulemavu wa ngozi
ndo maana aligombana na watu wa hapo wanakijiji
walikuwa wanasema Takadini anapaswa kuhuliwa.
Katika jamii yetu tunaona kuwa baadhi ya watu
wanawafanyia wezao ukatili
Katika kitabu cha, WATOTO WA MAMA NTILIE MWANDISHI
E-MBOGO
Migogoro kati ya Dani na Zita; pale wapi
walipo kuwa jaani walikuwa wanagombania mchele
ambao waliupata jaani na kwenda kupeleka
nyumbani hii inaonekana sio tabia nzuri kabisa
kwani inaweza kuleta madhara wakiwa huko jaani
kwa mfano kuchomwa na kitu kikali.
Migogoro kati ya Mzee Lomolomo na Mama
ntilie; huu ni pale ambapo mama ntilie ambapo
alikuwa anamkataza mzee lomolomo kunywa
pole na hafanye kazi nyingine lakini mzee
lomolomo alikataa kuacha pombe. Tunapaswa
~~tuwawa~~ ~~ku~~ tukiwa tunaambiwa tuwe tunu sikia


Kielelezo Na.11.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 11.

Katika Kielelezo Na. 11.2, mtahiniwa alishindwa kutoa mapendekezo sahihi ya kutokomeza rushwa katika jamii, hivyo kupata alama hafifu.

### 2.3.4 Swali la 12: Uhakiki wa Tamthiliya

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi,* mada ndogo ya *Uhakiki wa Tamthiliya* na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kuchambua maandishi katika tamthiliya teule. Swali lilimtaka mtahiniwa kuonesha jinsi ujinga wa wahusika ulivyozorotesha maendeleo katika jamii zao kwa kutoa hoja tatu kwa kila kitabu kupitia tamthiliya mbili walizosoma.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wengi zaidi ikilinganishwa na maswali mengine kutoka sehemu C ambapo watahiniwa (500,070) sawa na asilimia 95.78 walilijibu. Kiwango cha ufaulu kilikuwa kizuri zaidi ikilinganishwa na viwango vya ufaulu katika maswali mengine yote ya mtihani huu ambapo watahiniwa 450,870 (90.16%) walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 11 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 11**: *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 12.*

Katika Chati Na. 11, watahiniwa 49,200 (9.84%) walipata alama hafifu (0 hadi 4), watahiniwa 121,362 (24.27%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 4.5 hadi 9.5 na watahiniwa 329,508 (65.89%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama 10 hadi 15.

Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa asilimia 65.89 walijibu vizuri swali hili kwa kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu uhakiki wa tamthiliya teule. Watahiniwa hao waliweza kutoa hoja sahihi zinazoonesha jinsi ujinga wa baadhi ya wahusika ulivyozorotesha maendeleo katika jamii zao kwa kutumia tamthiliya teule. Watahiniwa hao walionesha umahiri wa uchambuzi wa fani katika tamthiliya teule ambapo waliweza kuonesha jinsi ujinga wa wahusika ulivyozorotesha maendeleo katika jamii kwa kuwatumia wahusika watatu kutoka kila tamthiliya mbili walizosoma. Ujinga wa wahusika kama vile *Furaha, Padre James* na *Mama Furaha* katika tamthiliya ya "Orodha", *Ngoswe, Mzee Kifaruhande* na *Mitomingi* katika tamthiliya ya "Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe" na *Joti, Suzi* na *Mama Suzi* katika tamthiliya ya "Kilio Chetu" ulioneshwa dhahiri jinsi ulivyokuwa kikwazo kwa maendeleo ya jamii husika. Aidha, watahiniwa hao waliandika utangulizi mzuri ulioeleza kwa kina maana ya *ujinga* na pia walitoa hitimisho zuri linaloendana na matakwa ya swali hili.

Kwa kutumia tamthiliya ya "Kilio Chetu" watahiniwa walionesha ujinga wa *Mama Suzi* ambaye hakumpa binti yake Suzi elimu ya jinsia kwa kufikiri kuwa bado ni mdogo. Hali hiyo ilimsababishia Suzi kupata mimba na kuacha shule. Aidha, walionesha ujinga wa *Suzi* wa kujiingiza kwenye mapenzi akiwa na umri mdogo, akapata mimba na hatimaye akafukuzwa shule. Pia walionesha ujinga wa Joti uliotokana na tabia yake ya kutembea na wasichana wengi na hatimaye kupata UKIMWI na mwishowe alifariki. Vivyo hivyo, kwa kutumia tamthiliya ya "Orodha" waliweza kuonesha ujinga wa *Furaha* wa kutokuwasikiliza wazazi wake hatimaye akapata mimba akiwa na umri mdogo. Vilevile, ujinga wa *Mary* ulimfanya kumshawishi rafiki yake *Furaha* kujiingiza kwenye ulevi na kutembea na bwana Ecko; na *Bwana Ecko* nae alionesha kuwa na ujinga kwani aliweza kuisaliti ndoa yake na kutembea na watoto wadogo hatimaye akaisababishia familia yake matatizo. Hali kadhalika, katika tamthiliya ya "Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe" watahiniwa hao walionesha ujinga wa wahusika *Mazoea* ambaye hakujua umuhimu wa nyaraka za sensa hivyo kutupa

mkoba wa Ngoswe walipokuwa wakitoroka pamoja, hali iliyosababisha karatasi zote za sensa zichomwe moto na Mzee Mitomingi na kuharibu zoezi zima la sensa. *Mzee Kifaruhande* ambaye hakujua umuhimu wa watu kuhesabiwa, hivyo kupuuza wito wa kusambaza habari za sensa kwa watu wa eneo lake, hivyo hawakuhesabiwa. Pia, walionesha ujinga wa Ngoswe wa kuchanganya ulevi, kazi na mapenzi uliosababisha kuchomwa kwa karatasi za sensa na kuharibu zoezi zima la kuhesabu watu na makazi. Kielelezo Na. 12.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri na kukidhi matakwa ya swali hili.

12. Ujinga ni ile hali ya mtu kutokuwa na elimu ya kitu chochote katika maisha yake au kimaendeleo ya jamii. Kwa kutumia tamthiliya mbili ya KILIO CHETU iliyoandikwa na MEDICAL AID FOUNDATION na tamthiliya ya ORODHA iliyoandikwa na STEVE REYNOLDS mwandishi ameweza kuwaonyesha wahusika ambao wamefanya ujinga kuwa ni chanzo cha maendeleo duni katika jamii.

Kwa kuanza na tamthiliya ya KILIO CHETU mwandishi amewatumia wahusika kwa kutoa hoja kama ifuatavyo:-

Mama Suzi, Mwandishi amemtumia mhusika huyu kwa kushindwa kutoa elimu ya kijinsia kwa mwanae Suzi hivyo Mama Suzi ameleta ujinga huu na kusababisha Suzi kuweza kupata mimba akiwa bado yupo shuleni na kusababisha maendeleo duni katika familia yake kwa sababu alishindwa kuendelea na masomo ili aweze kuikomboa familia yake hivyo Mama Suzi amesababisha maendeleo duni kwa ujinga wa kutompa mwanae elimu ya jinsia.

Suzi, Vilevile mwandishi ameweza kumuelezea Suzi kwa ujinga wa kujihusisha na mahusiano akiwa katika umri mdogo hivyo Suzi amesababisha maendeleo duni kwa sababu alishindwa kuendelea na masomo baada ya kupata mimba na kuweza kupoteza ndoto zake zote za kuendeleza maendeleo katika jamii yake na familia yake.

12. Joti; Mwandishi amewеza kumtumia mhu-
sika huyu kwa ujinga wa kuishi na wasichana-
wengi ambao waliweza kumpatia ugonjwa wa UK
IMWI ambao uliweza kuleta maendeleo duni kwa
familia yake ambao waliitaji kumsaidia kwa ku
mwaga pesa zao ili atibiwe na apone lakini ha
ikufanikiwa na Joti akapoteza maisha.
Kwa kumalizia na tamthiliya ya ORODHA
mwandishi amewatumia wahusika kwa kutoa hoja
kama ifuatavyo:-
Furaha; Mwandishi ameweza kumtumia-
mhusika Furaha kwa ujinga wa kutosikiliza man
eno ya wazazi wake hivyo ujinga huu ulimsab-
abishia Furaha kuweza kupata ugonjwa wa UKIM
WI ambao ulimpelekea kifo na kusababisha maend
eleo duni kwa familia yake baada ya kuondoka-
kwake na kuiacha familia yake.
Mery; Vilevile mwandishi amemtumia-
mhusika huyu kwa ujinga wa ulevi na kumsha-
wishi Furaha hivyo Mery amesababisha ujinga
huu kwake na kwa rafiki yake Furaha baada-
ya kumshawishi ~~am~~ atumie pombe na kama anaitaji-
awe mzuri basi aishi na Bwana Ecko hivyo-
mery amesababisha ujinga huu ambao ulimponza
rafiki yake Furaha.
Bwana Ecko; Mwandishi vilevile amemtu
mia mhusika huyu kwa ujinga wa kuisaliti ndoa-
yake na kwendwa kuishi na wasichana wadogo hivyo
Bwana Ecko alimbabisha maendeleo duni kwa famili
a yake baada ya kuanza kuisaliti.
Kwahiyo, Waandishi wote wawili wa tamth
iliya wamejitahidi katika kuonesha ujinga ambao
unaleta maendeleo duni kwa jamii kwa kuwatu-
mia wahusika tofautitofauti katika tamthiliya.

Kielelezo Na. 12.1: Sampuli ya jibu zuri katika swali la 12.

Katika Kielelezo Na. 12.1, mtahiniwa aliweza kubaini kwa usahihi ujinga wa wahusika mbalimbali na namna walivyozorotesha maendeleo katika tamthiliya ya "Kilio Chetu" na "Orodha" na

kupata alama za juu. Hata hivyo, mtahiniwa alikuwa na tatizo la kitahajia kwa kuandika *Mery* badala ya Mary kama jina hilo linavyosomeka katika tamthiliya ya "Orodha."

Baadhi ya watahiniwa (24.27%) waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango cha wastani kutokana na kutoa hoja zisizojitosheleza katika kuonesha jinsi ujinga wa wahusika ulivyozorotesha maendeleo katika jamii zao kupitia tamthiliya teule. Watahiniwa hao walionesha kuwa na uelewa usiojitosheleza kuhusu jinsi dhana ya ujinga ilivyotumiwa na waandishi wa tamthiliya teule. Baadhi yao walitoa hoja pungufu na wengine walishindwa kutumia mifano sahihi ya wahusika ambao ujinga wao ulizorotesha maendeleo katika jamii zao. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alimtumia *Padri James* na kuonesha ujinga wake wa kufanya ngono zembe na *Furaha* katika tamthiliya ya "Orodha" lakini alishindwa kuonesha jinsi ujinga huo ulivyozorotesha maendeleo katika jamii yao. Pia, watahiniwa wengine, kutokana na kukosa umahiri wa kuhakiki maudhui ya tamthiliya teule, walishindwa kujibu sehemu ya pili ya swali hili yaani kuonesha madhara ya ujinga wa wahusika katika tamthiliya teule, hivyo kupata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache (49,200) sawa na asilimia 9.84 ya waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu hafifu kutokana na kukosa umahiri kuhusu ujinga wa wahusika mbalimbali waliotumiwa na waandishi wa tamthiliya teule kwa lengo la kuonesha jinsi ujinga wao ulivyokuwa kikwazo cha maendeleo katika jamii zao. Watahiniwa hao walishindwa kubaini ujinga huo na kuonesha namna ulivyozorotesha maendeleo ya jamii kwa ujumla kwa kuwa walikuwa na uelewa mdogo wa uhakiki wa tamthiliya teule. Baadhi yao walibaini neno *ujinga* kama *taswira* zilizotumika katika tamthiliya teule na wengine walifafanua neno hilo katika muktadha wa *kisarufi* na kulibaini kama *nomino dhahania* kinyume na matakwa ya swali hili. Pia wapo watahiniwa waliobainisha dhamira mbalimbali katika tamthiliya hizo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitumia tamthiliya ya "Orodha" na kuandika, *chanzo cha UKIMWI* ni *kukosa maadili, kulewa* na *kutowasikiliza wazazi* lakini hakuunganisha wazo hilo na wahusika

waliopatwa na madhara hayo kutokana na ujinga wao, hivyo kupata alama hafifu.

Hali kadhalika, watahiniwa wengine walibainisha migogoro mbalimbali iliyojitokeza katika tamthiliya teule bila kuhusisha na ujinga wa wahusika na migogoro hiyo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alionesha mgogoro kati ya Suzi na mama yake baada ya Suzi kujiingiza kwenye mapenzi angali ni mwanafunzi katika tamthiliya ya "Kilio Chetu" lakini hakuonesha namna *ujinga* wa Suzi na mama yake ulivyoisababishia jamii yao kukosa maendeleo hususani Suzi kushindwa kuendelea na masomo. Kielelezo Na. 12.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kueleza jinsi ujinga wa wahusika ulivyozorotesha maendeleo katika jamii kupitia tamthiliya ya "Orodha" na "Kilio Chetu."

12. Ni kweli ujinga ni chanzo cha maendeleo
duni katika jamii. kwa kutumia vitabu viwili ambavyo
ni KILIO CHETU ambacho kimeandikwa na Medical Aid
foundation (TPH) na ORODHA ambayecho kimea
ndikwa na Steve Reynolds (MA).
kwa kuanza na kitabu cha KILIO CHE
TU ambacho kimeandikwa na Medical Aid founda
tion (TPH).
UKIMWI:- katika kitabu hiki tunaona
Joti alipata ukimwi Joti alikuwa angijihusisha na
mapenzi katika umri mdogo alikuwa anatemea na
watu wazima mfano chausiku. chausiku alikua amemzidi
Joti umri.
Kutokuwa muwazi:- katika kitabu hiki tunaam
uona Suzi hakuwa muwazi wa wazazi wake Suzi aliku
wa angijihusisha na mapenzi na joti tunaona pale suzi
alipokutwa na dawa za kuzuia mbi mimba kwen
ye mfuko wa sale za shule.

Mimba za Utotoni;- Tunaona pale Suzi alipata mimba na shule ikaishia hapo huyo Suzi alikuwa anamahusiano na Joti hapo Suzi akapata mimba bila kutalajia kwamba atapata mimba licha ya kwamba alikuwa ana kumeza dawa za ~~kodh~~ kuzuia mimba.

Kwa kumaliza na kitabu cha ORODHA ambacho Kimeandikwa na Steve Reynolds (MA).

Tamaa;- Tunamuona muhusika Furaha alikuwa na tamaa tunaona Furaha na rafiki yake walikuwa wanatoroka nyumbani usiku na kuelekea maeneo ya baa kwenda kwajili ya starehe.

Ukimwi;- Katika kitabu hiki muhusika Furaha aliambukizwa ukimwi pale walipo enda kule baa wakanya hadi wakalewa Furaha alitembea na Bwana Ecko bila yeye Furaha kujua hapondo alipata maambukizi ya ukimwi.

Umalaya;- tunaona mhusika Furaha na rafiki yake walikuwa wanafanya umalaya walikuwa wanatoroka nyumbani usiku na kwenda baa kwenda kutafuta wanaume.

Hitimisho:- Ujinga ni chanzo cha kutokuwa na maendeleo katika jamii mambo ambayo yanaifanya jamii kutopata maendeleo ni Ukimwi, Tamaa, Umalaya, Mimba za utotoni na kutokuwa muwazi.

Kielelezo Na. 12.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 12.

Katika Kielelezo Na. 12.2, mtahiniwa alieleza dhamira kama vile *UKIMWI, kutokuwa muwazi* na *mimba za utotoni* katika tamthiliya ya "Kilio Chetu" na *tamaa, UKIMWI* na *Umalaya* katika tamthiliya ya "Orodha." Aidha, mtahiniwa huyo alihitimisha kuwa uwepo wa dhamira hizo ndio chanzo cha maendeleo duni katika jamii bila kuhusisha ujinga wa wahusika kinyume na matakwa ya swali hili na kupata alama hafifu.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA

Mtihani wa somo la Kiswahili ulikuwa na maswali 12 yaliyotahiniwa kutoka mada sita ambazo ni *Ufahamu*, *Matumizi ya Sarufi*, *Utumizi wa Lugha*, *Uandishi*, *Maendeleo ya Kiswahili* na *Fasihi.* Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa katika mada mbalimbali unaonesha kuwa, watahiniwa walifaulu katika mada zote zilizotahiniwa mwaka 2022 ambapo mada mbili zilikuwa na ufaulu wa kiwango kizuri na mada nne kiwango cha wastani. Kiwango kizuri zaidi kilikuwa katika mada ya *Ufahamu* (87.64%) iliyotahiniwa katika swali la 8 na kufuatiwa na mada mchanganyiko (83.43%) katika swali la 1. Aidha, mada zilizokuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu zilihusisha *Fasihi* (60.78%) katika swali la 2, 4, 6, 10, 11 na 12; *Maendeleo ya Kiswahili* (46.24%) katika swali la 7, *Sarufi* (37.35%) katika swali la 3 na 5; na *Uandishi* (35.65%) katika swali la 9.

Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa katika mada mbalimbali kwa mwaka 2022 unaonesha kuwa mada nyingi zilishuka kiwango cha ufaulu katika mtihani huu ikilinganishwa na mwaka 2021. Mada zilizopungua kiwango cha ufaulu kwa kiasi kikubwa ni *Uandishi* kutoka asilimia 93.87 hadi 35.65 na *Sarufi* kutoka asilimia 65.35 hadi 37.35 ambapo zilipungua kwa asilimia 58.22 na 28 mtawalia. Mada hizi zinafuatiwa na mada za *Maendeleo ya Kiswahili* kutoka asilimia 49.74 hadi 46.24, *Mada mchanganyiko* kutoka asilimia 93.16 hadi 83.43 na *Fasihi* kutoka asilimia 67.59 hadi 60.78 ambazo pia zilipungua kwa asilimia 20.56, 9.73 na 6.81 mtawalia.

Ufaulu wa watahiniwa ulipanda katika mada moja pekee ambayo ni *Ufahamu* iliyokuwa na ongezeko la asilimia 11.96 kutoka asilimia 75.68 hadi 87.64. Ufaulu huu unaonesha kuwa, mada hii imepiga hatua kubwa kwani ufaulu wake ulipanda kwa mfululizo wa miaka mitatu tangu mwaka 2020 hadi 2022 ambapo kiwango cha ufaulu kilikuwa asilimia 43.3, 75.68 na 87.64 mtawalia.

Wastani wa ufaulu wa watahiniwa katika mada zote kwa mwaka 2022 ni asilimia 58.52. Kiwango hiki ni cha chini kwa asilimia 6.87 ikilinganishwa na mwaka 2021 ambapo wastani wa ufaulu wa mada ulikuwa asilimia 65.39.

Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika mada umeshuka kwa miaka mitatu mfululizo kuanzia mwaka 2020 hadi 2022 ambapo asilimia ya ufaulu ni 71.90, 65.39 na 58.52 mtawalia. Hali hii inaonesha kuwa katika mtihani huu, baadhi ya watahiniwa hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada mbalimbali zilizotahiniwa kwani walikuwa na ufaulu wa wastani hadi hafifu katika maswali mengi.

Kwa upande mwingine, mada zilizokuwa na kiwango cha chini cha ufaulu kwa mwaka 2022 zilikuwa ni *Uandishi* uliosababishwa na watahiniwa wengi kushindwa kuandika insha kwa usahihi, *Sarufi* ambapo walishindwa kufafanua taarifa za kisarufi katika viambishi tamati, kubaini miundo ya virai nomino na kuchanganua sentensi kwa njia ya jedwali. Aidha, katika mada ya *Maendeleo ya Kiswahili* kushuka kwa ufaulu kulitokana na watahiniwa wengi kushindwa kupendekeza namna ya kukuza na kueneza Kiswahili kwa wageni, pia ufaulu wa chini kwa mada ya *Fasihi* ulitokana na watahiniwa kushindwa kuthibitisha uhai wa fasihi simulizi na kutofautisha tanzu na vipera vya fasihi simulizi. Hivyo, jitihada zaidi zinahitajika katika ufundishaji na ujifunzaji wa mada hizi ili kuwajengea wanafunzi uelewa wa kutosha wa mada zote za somo la Kiswahili. Ufaulu wa watahiniwa katika mada mbalimbali kwa mwaka 2022 umeainishwa katika **Kiambatisho A**. Aidha, ulinganifu wa viwango vya ufaulu wa watahiniwa katika mada kwa mwaka 2021 na 2022 umeainishwa katika **Kiambatisho B**.

## 4.0 HITIMISHO

Kwa ujumla, Mtihani wa somo la Kiswahili wa mwaka 2022 ulizingatia Muhtasari wa somo la Kiswahili na maswali yote yalihusisha ngazi zote za majazi ya utambuzi yaani *kukumbuka, kuelewa, kutumia, kuchambua, kutathmini na kuunda*. Kiwango cha ufaulu kilikuwa kizuri, ambapo asilimia 95.58 ya watahiniwa walifaulu.

Uchambuzi umebainisha changamoto mbalimbali ambazo hazina budi kutatuliwa kama vile; kutofuatwa kwa maelekezo ya swali na uelewa mdogo wa baadhi ya mada hususani mada ya *Fasihi, Maendeleo ya Kiswahili, Sarufi* na *Uandishi*. Ili kuinua zaidi kiwango cha kufaulu kwa mada zote katika mtihani wa Kidato cha Nne, mikakati mbalimbali inahitajika katika mchakato

mzima wa ufundishaji na ujifunzaji ili kuwawezesha watahiniwa kupata ujuzi wa kutumia lugha kwa ufasaha na kukuza/kueneza lugha ya Kiswahili ndani na nje ya Tanzania hasa ikizingatiwa kuwa Lugha ya Kiswahili inayo hadhi kubwa Kitaifa na Kimataifa, hivyo, sharti ifahamike na kutumika ipasavyo.

Hata hivyo, uchambuzi huu unaonesha kuwa, zipo mada zinazohitaji jitihada za dhati katika ufundishaji na ujifunzaji. Hii ni kwa sababu kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika mada chache umeonekana kuwa na changamoto hususan kwa maswali yaliyohitaji umahiri wa juu wa kufikiri wa mtahiniwa. Hivyo, mada za *Fasihi, Maendeleo ya Kiswahili, Sarufi* na *Uandishi* zinapaswa kutiliwa mkazo ili ziwe na ufaulu mzuri wakati ujao. Licha ya mada hizo kuwa na ufaulu wa wastani, mada ya *Uandishi* (35.65%) ilikuwa na ufaulu wa chini zaidi kwa mwaka 2022 kwani ufaulu umeshuka kwa asilimia 58.22 ikilinganishwa na mwaka 2021 ambapo ufaulu ulikuwa asilimia 93.87.

Taarifa hii itasaidia kuinua zaidi kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika somo la Kiswahili na kutatua changamoto kwa walimu na wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa mada mbalimbali. Pia, taarifa hii itawafanya walimu na wanafunzi kuyaelewa makosa mbalimbali yanayojitokeza wakati wa kujibu maswali ya mtihani na kufanya maboresho katika mfumo mzima wa ufundishaji na ujifunzaji kwa lengo la kuinua kiwango cha ufaulu kwa kipindi kijacho.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuinua zaidi kiwango cha ufaulu katika mada za *Fasihi*, *Maendeleo ya Kiswahili, Sarufi* na *Uandishi* kutoka ufaulu wa wastani kuwa ufaulu mzuri inashauriwa kuwa:

(a) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa maswali, majibu na majadiliano ili kufafanua dhima ya uambishaji katika vitenzi vya Kiswahili.

(b) Kwa kutumia onesho mbinu na chati ya tungo, mwalimu awaongoze wanafunzi kubaini na kufafanua aina za virai na dhima zake katika mawasiliano. Pia, waongozwe kuchanganua sentensi kwa njia ya matawi na majedwali.

(c) Wanafunzi wajadili katika vikundi sifa na tanzu za fasihi simulizi. Aidha, mwalimu awaongoze kwa maswali na majibu ili kubaini vipera vya fasihi simulizi.

(d) Kwa njia ya bungua bongo, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza jinsi Kiswahili kinavyoweza kuenezwa kwa wageni kupitia biashara, utawala, utamaduni na mafunzo mbalimbali.

(e) Wanafunzi washiriki kivikundi katika majadiliano ili kubaini taratibu za uandishi wa insha za hoja na kufanya mazoezi ya uandishi wa insha mbalimbali.

## KIAMBATISHO A: UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA MWAKA 2022

| Na. | Mada | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Ufaulu (%) | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Na. ya Swali | % ya Ufaulu (alama 30+) | | |
| 1. | *Ufahamu* | 8 | 87.64 | 87.64 | Vizuri |
| 2. | *Sarufi, Utumizi wa Lugha, Uandishi na Fasihi kwa Ujumla (Swali la Kuchagua)* | 1 | 83.43 | 83.43 | Vizuri |
| 3. | *Fasihi* | 2 | 62.43 | 60.78 | Wastani |
| | | 4 | 23.74 | | |
| | | 6 | 21.47 | | |
| | | 10 | 79.23 | | |
| | | 11 | 87.62 | | |
| | | 12 | 90.16 | | |
| 4. | *Maendeleo ya Kiswahili* | 7 | 46.24 | 46.24 | Wastani |
| 5. | *Sarufi* | 3 | 35.38 | 37.35 | Wastani |
| | | 5 | 39.32 | | |
| 6. | *Uandishi* | 9 | 35.65 | 35.65 | Wastani |

**KIAMBATISHO B: ULINGANIFU WA UFAULU KATIKA MADA MWAKA 2021 & 2022**

